

# Kuhamia Finlande

## Uongozi wa Sehemu ya Wakimbizi Wanaohamia Inchi ya Finlande

mof.fi

Maahanmuuttovirasto
Migrationsverket
Finnish Immigration Service

IOM
UN MIGRATION

ASYLUM, MIGRATION AND INTEGRATION FUND
Supported by the European Union

**Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande (Migri)** ni shirika la kiserikali chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Inashurulikia na kufanya maamuzi kuhusu mambo yanayohusiana na uhamiaji, nyumba, mambo ya wakimbizi na uraia wa Finlande. Migri pia inaamua kuhusu kesi za kawaida, dharura na haraka za nyumba zinazopelekwa kwa Finlande na UNHCR na ina kazi la jumla kuhusu mpango wa mwelekeo wa kitamaduni unaopangwa kwa ajili ya wakimbizi walio tayari inje ya inchi mbele ya kuhama kwa Finlande.

**Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM)** ni Shirika Linalohusiana na Umoja wa Mataifa, na shirika linaloongoza la Umoja wa Mataifa katika uwanja wa uhamiaji. IOM imejitolea kwa kanuni ya utu kwamba uhamiaji unayoangalia ubinadamu na utaratibu unayoleta faida kwa wahamiaji na jamii.


**WACHAPISHAJI**

**Utumishi ya Uhamiaji ya Finlade (Migri)**
Opastinsilta 12 A
SANDUKU LA BARUA 10
00086 Maahanmuuttovirasto
Finlande
Site: migri.fi
Musimamizi wa Muradi: Marjo Mäkelä

**Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM)**
Ofisi ya Inchi katika Finlande
Unioninkatu 13, Ghorofa ya 6
SANDUKU LA BARUA 851
00101 Helsinki
Finlande
Site: finland.iom.int
Mwongozi wa Muradi: Julia Jänis
Mushauri Akseli Saviranta

Kutengeneza jengo ya site: Sopiva Design
Kutengeneza picha ya jalada: Sopiva Design



Haki zote zimelindwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kutolewa tena, kubadilishwa, au kusambazwa kwa hali chochote au kwa njia yoyote ya, elektroniki, kimitambo, kuchapisha, kurekodi, au vinginevyo bila ruhusa ya maandishi ya mchapishaji.



Muradi huu (ikiwa ni pamoja na uongozi huu) unasimamiwa na Umoja wa Ulaya, Feza za Kimbilio, Uhamiaji na Ushirikiano.


SWAHILI

Maahanmuuttovirasto
Migrationsverket
Finnish Immigration Service

IOM
UN MIGRATION

ASYLUM, MIGRATION AND INTEGRATION FUND
Supported by the European Union

# Kuhamia Finlande

**Uongozi wa Sehemu ya Wakimbizi Wanaohamia Inchi ya Finlande**

mof.fi

**Pata barua hii mtandaoni katika**
**mof.fi/welcome**
**ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

# Yaliyomo


**Utangulizi ........ 5**
- Faida ya Kutumia Uongozi wa Kuhamia Finlande . . . . 5
- Jinsi ya Kutumia Uongozi wa Kuhamia Finlande 5
- Faida ya Kutumia Uongozi wa Kuhamia Finlande . . . . 6
- Maulizo Yanayoulizwa Sana. . . . . 7
- Mambo ya Kusaidia . . . . 8

**Utangulizi wa Jamii ya Finlande ........ 9**
- Nafasi ya Kijiografia na Idadi ya Watu . . . . 11
- Hali ya Hewa . . . . 13
- Majimbo na miji. . . . . 15
- Njia Kubwa ya Kupata Vyakula . . . . 17
- Mazoea ya Kitamaduni. . . . . 18
- Nafasi za Jamaa . . . . 19
- Kuwa Finlande kama Mhamiaji. . . . . 20
- Majibu . . . . 25

**Kujitayarisha – Kujitayarisha Kwa Kuishi kwa Finlande ........ 29**
- Kujitayarisha kwa Uhamiaji wa Kudumu. . . . . 31
- Barua za Usafiri na Vyeti Vingine . . . . 33
- Masomo na Mpango wa Kutafuta Kazi . . . . 34
- Kujiandaa Kiakili kwa Uhamiaji. . . . . 35
- Kuzoea Tamaduni Mpya. . . . . 36
- Majibu. . . . . 49

**Usafiri – Kwenda Finlande ........ 51**
- Kujitayarisha kwa Safari ya Ndege. . . . . 53
- Katika Uwanja wa Ndege. . . . . 57
- Kufika . . . . 58
- Majibu . . . . 60

**Maisha ya kila siku – Kushurulikia Maisha ya Kila Siku ........ 63**
- Nyumba za Kupanga . . . . 65
- Facture . . . . 66
- Kanuni na Sheria za Kawaida . . . . 68
- Usafi na Taka . . . . 69
- Ununuzi katika Eneo Yako . . . . 71
- Benki. . . . . 72
- Usafiri . . . . 73
- Uvutaji Sigara. . . . . 75
- Majibu . . . . 76

**Masomo – Shule na Masomo ........ 79**
- Utumishi ya Utunzaji wa Watoto na Masomo ya Mbele ya Shule ya Msingi . . . . 81
- Shule ya Jumla. . . . . 81
- Shule ya Sekondari ya Juu . . . . 85
- Majifunzo ya Maneno ya Kiufundi . . . . 85
- Masomo ya Juu na Vyuo Vikuu . . . . 86
- Majifunzo ya Uingizaji kwa Wahamiaji. . . . . 88
- Masomo ya Kiufundi na Majifunzo kwa Watu Wazima na Majifunzo kwa Soko la Kupata Kazi kwa Watu Wazima. . . . . 88
- Utambuzi rasmi wa Masomo na Diplomes zilizopatwa InNje ya Inchi . . . . 90
- Pahali pa Kusoma Vitabu na Shuruli za Nyuma ya Masomo . . . . 91
- Majibu . . . . 92

**Kazi – Kufanya Kazi katika Finlande ........ 95**
- Mpango wa Kuingia na Majifunzo kwa Wahamiaji . . . . 97
- Utafutaji Kazi . . . . 100
- Ushuru . . . . 104
- Mapashwa na Haki Zako . . . . 106
- Utamaduni wa Kazi katika Finlande. . . . . 107
- Majibu . . . . 110

**Kusimama – Utumishi za Afya na Utumishi za Kusimama wa Jamii ........ 113**
- Utumishi za Afya . . . . 115
- Kusimama wa Jamii. . . . . 118
- Usaidizi kwa Kuingia. . . . . 119
- Majibu . . . . 120

**Luga – Utangulizi wa Luga ya Kifinlande .. 123**
- Mazoezi . . . . 125
- Majibu . . . . 136

**Viungo – Site Zaidi Muhimu za Kutembelea .... 143**
- Utumishi za Jamii na Maelezo kuhusu Finlande . . . . 145
- Kazi na Masomo . . . . 147
- Kusimama na Haki . . . . 148
- Jamaa, Watoto na Vijana . . . . 149
- Mengine . . . . 150

# Utangulizi

Uongozi huu umeandaliwa na Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji, IOM, kwa uangalifu mkubwa ili kukusaidia uanze safari yako kama sehemu inayokubaliwa ya wakimbizi wanaohamia inchi ya tatu wapi watapewa pahali pa kuishi katika Finlande. Tafazali beba kitabu chako cha kazi unaposafiri kwenda Finlande; kinaweza kukusaidia sana katika hali tofauti unapoishi na kujifunza kuzoeshana na jamii mpya.

Uongozi huu umetayarishwa tu kwa sehemu ya wakimbizi wanaohamia inchi ya tatu na haiko kwa wale wanaofikilia au wanaojiandaa kuhamia Finlande kwa sababu zingine zisipokuwa pahali mpya ya kuishi. Sehemu ya wakimbizi wanaohamia nchi ya tatu ina hali ya kisheria ambayo ni tofauti na wakimbizi wengine au watu wengine wanaohamia Finlande kwa madhumuni mengine, kwa hivyo maelezo katika uongozi huu hasa hayawahusu.

## Faida ya Kutumia Uongozi wa Kuhamia Finlande

Uongozi huu unapatikana katika miundo mingi. Uongozi huu unaweza kuchapishwa au kutumiwa kwa mfano kwenye simu yako, ordinateur.

Ikiwa ungependa kuangalia au kupata uongozi, enda kwenye site ya Kuhamia kwa Finlande na uandike adresse mof.fi kwenye fasi ya adresse, na uchague la luga yako. Unaweza kupata sura moja kwenye mof.fi ukienda kwa sehemu ya site ile unataka na kufinya kiungo cha utafutaki kilicho hapo. Kwa mfano, ikiwa ungependa kutafuta sehemu ya Maisha ya Kila Siku, finya kiungo cha Maisha ya Kila Siku, enda chini ya ukurasa na ufinye kiungo cha utafutaji kwenye rangi ya majifu. Katika uongozi huu, kwa mwanzo wa kila sehemu, pia kuna kiungo kinachoweza kutumiwa kupata sehemu mtandaoni.

Ili kupata ile sehemu, lazima uunganishwe kwa internet. Ikiwa kuna garama yoyote inayohitajika ili kufikia internet, ni jukumu lako kuzilipia. Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande haitalipa garama hizi. Unapokuwa Finlande, unaweza kutumia muunganisho wa internet unaopatikana kwenye pahali pa kusoma vitabu ya jamii.

## Jinsi ya Kutumia Uongozi wa Kuhamia Finlande

Uongozi umegawanywa katika sehemu tisa. Sehemu hizi ni Finlande, Kujiandaa, Kusafiri, Maisha ya Kila Siku, Masomo, Kazi, Kusimama, Luga, na Viungo.

Kila sehemu inashurulikia jambo fulani, na inakupa maelezo ya msingi ambayo unaweza kujifunza na kuzungumuzia. Kila sehemu inaangazia jambo tofauti na nyingine. Hata hivyo inashauriwa upitie sehemu nyingi iwezekanavyo ili uelewe vizuri kujiingiza kwako katika jamii.

Kila sehemu ina rangi yake. Ukurasa wa kwanza wa kila sehemu una viungo vya sehemu ya somo na sehemu ya mazoezi; zote zinapatikana mtandaoni kwenye site ya Kuhamia Finlande.

Sehemu zinakuwa na mazoezi mbalimbali na kazi za kuongeza. Kuna aina tofauti za mazoezi. Kwa mfano, katika ya mazoezi zingine unahitaji kusoma na kujibu maulizo, katika zingine una majibu mbalimbali ya kuchagua, na katika zingine unahitaji kufikilia

na kuzungumuza na wengine wakati wa majifunzo ya kabla ya kuondoka. Kila zoezi lina maagizo ya kufuata.

Mazoezi yataimarisha hali yako ya ujifunzaji na maarifa kuhusu Finlande. Kazi ya kuongeza zitakupa maelezo zaidi na kuimarisha maarifa yako kujua zaidi. Unaweza kufanya mazoezi na kazi zilizoongezwa peke yako, kwa kikundi au pamoja na msimamizi wako wakati wa majifunzo ya mbele ya kuondoka.

Majibu ya mazoezi ya sehemu yanaweza kupatikana kwa mwisho ya kila sehemu.

Katika kila sehemu, unaweza kupata namba ya siri ya Jibu la Haraka (QR). Alama ya QR unakaa hivi:

Alama ya QR ni viungo kwa aina ya picha, na inaweza kutumiwa kufikia site. Ili kufikia site kupitia alama ya QR, lazima uunganishwe kwenye internet.

Unaweza kufunua alama ya QR kwa kutumia kamera ya simu yako. Kwa simu zingine, unahitaji programme tofauti ya kusoma alama ya QR. Kwenye Android, unaweza kuweka programme ya kusoma alama wa QR kutoka duka la Google Play. Kwa iPhone, unaweza kuweka programme ya kusoma alama ya QR kutoka kwa App Store. Kwa Windows Phone, unaweza kuweka programme ya kusoma alama ya QR kutoka kwa Windows App Store. Kwa Sailfish OS, unaweza kuweka programme ya kusoma alama ya QR kutoka hazina ya Sailfish App Repository au hazina zingine. Fungua programme ya kusoma alama ya QR na uendelee na maagizo.

## Faida ya Kutumia Uongozi wa Kuhamia Finlande

Kama sehemu ya wakimbizi wanaohamia inchi ya tatu, unaweza kutumia uongozi huu kabla, wakati, na baada ya majifunzo ya kabla ya kuondoka. Tunakushauri sana ujifunze uongozi huu kwa uangalifu. Uongozi huu pia umetengenezwa ili kukutia moyo kujifunza wewe mwenyewe. Unaweza kupata uongozi huu wakati wowote mtandaoni kwa kuandika mof.fi katika kwa internet, utaongozwa kwenye site ya Kuhamia Finlande. Unapotumia uongozi huu, rejelea kila wakati site ya Kuhamia Finlande ambapo utapata maelezo zaidi kuhusu Finlande.

Unashauriwa sana uanze kujiandaa kwa pahali yako mpya ya kuishi, na uongozi huu ni moja ya njia ambazo Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande inakupa ili utengeneze vizuri namna kujifunza kwako. Mazoezi mengi yanaweza kufanywa na kila mtu bila kujali umri, jinsia, kiwango cha masomo, au jambo lingine lolote. Mazoezi mengine yanaweza kuwa magumu na mengine kuwa rahisi - jinsi tu safari yako ya kuhamia Finlande itakavyokuwa.

Kumbuka kwamba juhudi zako za ujifunzaji zitakuwa ya maana na zitasaidia mwanzo wa maisha yako mapya katika inchi yako mpya.

Hebu tuanze kujifunza kuhusu Finlande na luga ya Finlande.

# Maulizo yanayoulizwa sana

## 1. Ninaweza kujifunza wapi luga ya Finlande?

Unaweza kujifunza sehmu ya luga ya Finlande katika sehemu ya luga. Ama, unaweza kwenda katika mof.fi
na kisha utembelee sehemu ya luga. Utapata viungo vingi ambavyo vitakusaidia katika maendeleo yako ya kujifunza. Unaweza kutembelea site kabla na baada ya kupata pahali pako mpya katika Finlande. Inashauriwa uanze kujifunza luga mapema iwezekanavyo, tayari kabla ya kuhamia Finlande.

## 2. Je, ninaweza kupata wapi maelezo kuhusu kazi?

Unaweza kupata maelezo kuhusu kazi katika sehemu ya kazi.

## 3. Siwezi kupata viungo vya kupakua uongozi. Nifanye nini?

Viungo vinapatikana kwa mwanzo ya kila sehemu. Unaweza kuandika adresse kwa internet ao utumie alama ya QR. Angalia sehemu ya Jinsi ya Kutumia uongozi wa Kuhamia Finlande ikiwa unahitaji usaidizi zaidi.

## 4. Site haipatikani. Nifanye nini?

Angalia muunganisho wako wa internet na ujaribu kutembelea site tena baada ya muda mfupi.

## 5. Sikuweza kufanya mazoezi yote. Nifanye nini?

Unaweza wakati wote kujaribu kufanya mazoezi tena wakati una muda. Inashauriwa sana kwamba ufanye mazoezi yote na usome majibu yaliyotolewa. Unaweza kuzungumuza na rafiki ao na mutu wa jamaa na uwaombe usaidizi ikiwa unauhitaji.

## 6. Nilifanya mazoezi yote. Ninaweza kupata wapi zaidi?

Tembelea mof.fi na uangalie sehemu za luga na viungo. Je, ulifanya pia kazi zote zilizoongezwa, ambazo zinaweza kupatikana katika sehemu zingine?

## 7. Je, ninaweza kushiriki uongozi huu?

Uongozi huu umekusudiwa kwa sehemu ya wakimbizi wanaohamia inchi tatu na haukusudiwi kwa wakimbizi wengine ao watu wengine wanaohamia Finlande kwa sababu zingine. Kwa hivyo maelezo yaliyotolewa hapa sio lazima itumike kwao.

# Maelezo

Isipokuwa imeelezwa namna ingine, picha zinazopatikana katika uongozi huu zinapatikana katika miliki ya uma. Iwapo imeelezwa namna ingine, picha ni mali ya wachapishaji wake na zinapatikana tu katika uongozi huu kwa ajili ya kujifunza.

Uongozi unatoa maelezo ya kimsingi kuhusu Finlande kupitia mifano na mazoezi. Majibu yanaweza kutofautiana na sio yote yametajwa. Ingawa kila juhudi imefanywa ili kuhakikisha kuwa maelezo ni ya hivi karibuni, Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji hawakubali wajibu wowote wa uharibifu wowote wa moja kwa moja ao usio wa moja kwa moja unaotokana na makosa yanayowezekana katika yaliyomo. Kwa kuongezea, Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji hawahusiki kwa vitu vinavyotolewa na mashirika ya inje ijapokuwa ya kutoa viungo vinavyoelekea kwao.

Maoni yaliyotolewa katika chapisho hili ni ya waandishi na hayielezi maoni ya Shirika la Kimataifa la Uhamiaji ao Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande. Utaalamu uliotumika na kutoa vitu wakati wote wa uchapishaji hauonyeshi uelezaji wa maoni yoyote kwa upande wa IOM ao Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande kuhusiana na hali ya kisheria ya inchi yoyote, wilaya, jiji ao eneo, ao mamlaka yake, ao kuhusu mipaka yake.

Hakimiliki za uongozi huu ni ya Utumishi ya Uhamiaji ya Finlande na zinashirikiwa na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji. Uongozi huu unaweza kutajwa ikiwa utataja Utumishi ya Uhamiaji ya Kifini.

# Finlande

**Utangulizi wa Jamii ya Finlande**



Je, inchi ya Finlande iko wapi? Je, watu wa Finlande wako namna gani?
Haki na mapashwa ya wakaaji wa Finland ni gani?
Katika sura hii, utajifunza kuhusu haya na mengine.

**Katika sehemu hii, utajifunza kuhusu:**

- Eneo la kijiografia na idadi ya watu
- Hali ya hewa
- Majimbo na miji
- Njia kubwa ya kupata vyakula
- Mazoea ya kitamaduni
- Nafasi za wanamemba ya jamaa
- Kuwa Finlande kama mhamiaji

**Soma kuhusu sehemu hii katika mof.fi/sections/finland/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

**Pata sehemu hii mtandaoni katika mof.fi/exercises/finland/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

# Eneo la kijiografia na idadi ya watu

Nchi ya Finlande iko katika sehemu ya kaskazini ya ulimwengu na kati ya Uswidi na Urusi. Kwa kaskazini, Finlande inashiriki mpaka na Norwe. Estonia iko upande wa kusini mwa Finlande. Luga rasmi nchini Finlande ni Kifinlandi na Kiswidi. Hesabu ya watu wa Finlande ni karibu watu milioni 5.5. Kuna karibu wazungumzaji 250,000 wa luga za kigeni inchini.

**1.** Kutoka kwa maandishi, weka alama ya mdmviringo kwa inchi ambayo ao ambazo ni majirani wa Finlande?

Estonia | Urusi | Uswidi | Ufaransa | Ujerumani | Kanada | Norwe

**2.** Je, unafahamu jina la bara ambalo Finlande inapatikana?

______________________________

______________________________

**3.** Kuna ramani kwenye ukurasa ufuatayo. Weka alama katika eneo la Finlande kwa ramani.

**4.** Kwa ramani hiyo hiyo, chora njia kutoka eneo lako la sasa kwenda Finlande. Kulingana na maoni yako, safari ya ndege inachukua muda gani kutoka eneo lako la sasa kwenda Finlande? Zungumuzia hili pamoja na jamaa yako ao wenzako.

**5.** Kwenye ramani hiyo hiyo, chora njia zingine ambazo umepitia katika inchi zingine.

**!**


- Finlande iko kwa Ulaya ya Kaskazini.
- Majirani wa Finlande ni inchi za Uswidi, Norwe, Estonia na Urusi.
- Luga ya kazi katika Finlande ni Kifinlande na Kiswidi;
  hata hivyo Kifinlande kinazungumzwa na watu wengi zaidi.



# Hali ya Hewa


**Finlande ina nyakati ine tofauti: kuchipua (printemps), kipwa, kupukutika (automne) na baridi. Kila moja ya nyakati una mahitaji yake ya mavazi na shuruli mbalimbali za inje.**

1. Sasa tuangalie picha zinazopatikana hapo chini. Ni gani ambayo haikuchukuliwa inchini Finlande?
2. Je, hali ya hewa ni tofauti na inchi yako ya nyumbani ao inchi ya sasa?
   Je, unazani hali ya hewa inaweza kugusa namna gani maisha yako ya kila siku inchini Finlande?


a


b


c


d


e


f


g



h


i


j


k


l


m



n


o

# Majimbo na miji

**1.** Sasa tuangalie ramani. Majina ya majimbo na ya miji chache ziko hapo chini.

**1** Uusimaa
**2** Varsinais-Suomi
**3** Satakunta
**4** Kanta-Häme
**5** Pirkanmaa
**6** Päijät-häme
**7** Kymenlaakso
**8** Etelä-Karjala
**9** Etelä-Savo
**10** Pohjois-Savo
**11** Pohjois-Karjala
**12** Keski-Suomi
**13** Etelä-Pohjanmaa
**14** Pohjanmaa
**15** Keski-Pohjanmaa
**16** Pohjois-Pohjanmaa
**17** Kainuu
**18** Lappi
**19** Ahvenanmaa






Sasa tuangalie alama za majimbo.



Finlande imegawanywa katika majimbo, na kila jimbo umegawanywa katika miji. Katika zoezi hili, utajifunza kuhusu nafasi na sifa za kila jimbo na pia nafasi ya miji mingine. Utafanya hivyo ukusoma maelezo ya miji yanayopatikana hapo chini na kuangalia alama zinazopatikana kwa ukurasa uliopita. Jaribu kufahamu alama ya kila muji. Sasa tusome maelezo yote mbele ya kuanza.

**a.** **Ahvenanmaa**: Ni jimbo ndogo zaidi katika Finlande, na unajitawala na hauna mamlaka ya kuwa na majeshi. Alama yake ndio pekee ambayo ina aina ya nyama kama ayala.

**b.** **Etelä-Karjala**: Alama hiyo ina panga mbili. Lappeenranta iko katika eneo hili.

**c.** **Etelä-Pohjanmaa**: Seinäjoki iko katika mkoa huu. Alama hiyo ina cheche nyingi nyeupe na nyuma yake ni ya rangi ya samawi (bleu)

**d.** **Etelä-Savo:** Alama ina upinde na mshale unaoelekea kulia, na jimbo hii ni jirani ya Kymenlaakso. Ziwa kubwa zaidi inchini Finlande, Ziwa Saimaa, iko hapa.

**e.** **Kainuu**: Alama inafanana na ile ya Pirkanmaa lakini ina rangi ya kijani kuliko ya nyekundu. Kajaani iko hapa.

**f.** **Kanta-Häme**: Hämeenlinna ndio jiji kuu ya jimbo hili. Alama ina nyota tatu, maua ine nyeupe, na nyama.

**g.** **Keski-Pohjanmaa**: Alama ina cheche moja. Kokkola iko hapa.

**h.** **Keski-Suomi**: Alama hiyo ina ndege nyeusi. Jyväskylä iko hapa.

**i.** **Kymenlaakso**: Alama ina samaki. Kotka iko hapa.

**j.** **Lappi**: Alama hii ni ya jimbo mkubwa zaidi na ni kwa kaskazini zaidi, ambapo Rovaniemi inapatikana.

**k.** **Pirkanmaa**: Rangi pekee katika alama hii ni nyekundu na manjano. Tampere iko hapa.

**l.** **Pohjanmaa**: Alama hii ina cheche nyekundu. Vaasa iko hapa.

**m.** **Pohjois-Karjala**: Alama ina panga mbili na taji. Ziwa Hattuvaara, ambalo ni sehemu ya mashariki zaidi katika Finlande na eneo la Schengen, iko hapa.

**n.** **Pohjois-Pohjanmaa**: Alama ina idadi mara mbili ya cheche ikilinganishwa na jirani yake ya kusini. Oulu iko hapa.

**o.** **Pohjois-Savo**: Alama ina upinde na mshale. Kuopio ndio jiji kubwa zaidi katika jimbo hili.

**p.** **Päijät-Häme**: Alama ina nusu mutu nusu samaki na ndege. Lahti iko hapa

**q.** **Satakunta**: Alama ina nyama ameshika upanga. Pori iko hapa.

**r.** **Uusimaa**: Alama ina mashua. Helsinki iko katika jimbo hili

**s.** **Varsinais-Suomi**: Alama ina bendera mbili za samawani na manjano. Turku iko katika jimbo hili.

!

- Finlande ni inchi kubwa, na kila jimbo katika Finlande ina fasi zake maalum na historia yake.
- Utakuwa ukiishi katika muji. Miji zote zinatoa utumishi za kuingiza kwa wageni kuzoea.

# Njia kubwa ya kupata vyakula

Je, kwa sasa unajua Finlande kwa kiasi gani, watu, utamaduni, na uchumi wake? Hebu tusome maulizo yanayopatikana hapo chini na tuyajibu.

**a.** Je, Finlande na Uswidi ndizo jamhuri pekee kati ya inchi za Kaskazini?

______________________________

**b.** Je, Finlande hutumia yuro kama makuta?

______________________________

**c.** Je, mashine na mbao ni vitu muhimu vinavyouzwa ya inje kwa Finlande?

______________________________

**d.** Je, utumishi za misitu unatoa kazi kwa watu wa Finlande wengi siku hizi?

______________________________

**e.** Je, shirika za kiteknolojia na utumishi zinaleta kazi kwa watu wengi inchini Finlande?

______________________________

**f.** Je, kuna watu milioni kumi wanaoishi Finlande?

______________________________

**g.** Je, watu wa asili ya Kifinlande wanatumia jina tofauti kwa Finlande?

______________________________

**h.** Je, Kizungu ni luga rasmi inchini Finlande?

______________________________

**i.** Je, kuna mchezo unaoitwa kandanda ya kinamasi katika Finlande?

______________________________

!

- Sehemu kubwa ya eneo la jumla la udongo ya Finlande limefunikwa na misitu.
- Shirika za kiteknolojia na utumishi zinaleta kazi kwa watu wengi.

# Mazoea ya kitamaduni

Hebu tuangalie tena ukurasa wa site ya somo. Kiungo kinaweza kupatikana kwa mwanzo ya sehemu hii. Umeiipata? Inakaa hivi mof.fi/sections/finland/en na unaweza kupata maelezo mengi ambayo yatakusaidia kupata maneno yanayokosekana katika zoezi hili.

**a.** Kupeana mkono na ______________________________ ni njia ya kawaida ya kusalimiana katika Finlande.

kutikisa kichwa kukumbatiana kugusana pua

**b.** Watu wa Finlande kawaida wanaanza mazungumzo na mgeni kwa ____________________________.

haraka umakini

**c.** Kwa sababu hii watu wa Finlande wanaweza kuonekana kama wenye haya na ______________________. Kawaida Watu wa Finlande hawaombi muda murefu ya kuzungumza katika mkutano ya watu wengi na kawaida wanaeleza kusudi kwa haraka.

furaha ujeuri wasiyo na adabu

**d.** Usawa na haki ni mambo muhimu kwa watu wa Finlande. Pia, watu wa Finlande wanaona udamani katika uaminifu na kuweka ________________________. Kufanya kazi na kuwa na bidii ni ya damani sana. Kufuata wakati na kuchunga nyakati zilizokubaliwa ni muhimu.

nafasi ya kibinafsi kujitenga ahadi

**e.** Watu wachache inchini Finlande wanatumia pombe nyingi sana katika ___________________________ na siku kuu maalum za sherehe, jambo ambalo linaweza kuwachanganya wahamiaji. Matumizi ya pombe kupita kiasi yanaweza kusababisha magonjwa na mizozo katika jamaa.

siku ya kwanza ya mwezi siku ya kwanza ya wiki wikendi

**Kazi ya kuongeza!**
Siku ya Uhuru ya Finlande ni tarehe 6 Septemba.
UKWELI UONGO

!

- Ya damani kwa Finlande ni pamoja na usawa, haki na uaminifu.
- Ubaguzi na unyanyasaji haziruhusiwi hata kidogo.
- Kufuata muda ni ya damani sana, katika mambo ya kitaalamu na kibinafsi.

# Nafasi za wanamemba ya jamaa

**Katika Finlande, mipangilio na aina za jamaa hutofautishaana na inaweza kuwa tofauti na jinsi ambavyo umezoea.**

**1.** Katika zoezi lifuatalo, utatembelea ukurasa wa site kupitia kiungo au kwa kusoma alama wa QR na usome kuhusu usawa inchini Finlande. Ukurasa za sites uko kwenye site inayoitwa InfoFinland. Inashauri sana utembelee InfoFinland kwa sababu inatoa maelezo muhimu.

infofinland.fi/en/information-about-finland/finnish-society/equality-and-non-discrimination

Hebu tuchore mshale ili kuunda tangamano inayoelezea kitu ambacho umechosoma kutoka kwa maandishi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | Kulingana na sheria ya Finlande, wanaume na wanawake | daima ni uhalifu. | **u** |
| **b** | Mshahara wa juu haupaswi kulipwa kwa mwanaume | kulingana na wakati maamuzi yanayowahusu yanapofanywa. | **v** |
| **c** | Watoto wana haki ya maoni yao | ni marufuku na inaweza kusababisha gazabu. | **w** |
| **d** | Unyanyasaji ambao unafanyika katika jamaa na katika uhusiano, kama vile unyanyasaji wa kimwili na kingono, | wana haki sawa. | **x** |
| **e** | Kulingana na sheria ya Finlande, kupiga watoto | bila usawa na ujumuishaji. | **y** |
| **f** | Suluhisho kwa matatizo ya ulimwengu hazitapatikana | ikilinganishwa na mwanamke kwa misingi ya jinsia. | **z** |

**Kazi ya kuongeza!**
Ni mwaka gani Finlande ilikuwa inchi ya kwanza ulimwenguni kupitisha sheria inayowaruhusu wanawake kupiga kura na kugombea uchaguzi?
1906 1926 1946

- Wanawake na wanaume, wavulana na wasichana wanachukuliwa kuwa sawa inchini Finlande.
- Watoto ao mtu yeyote hawezi kuazibiwa na aina yoyote ya unyanyasaji; hawawezi kupigwa, kupigwa makofi, kuvutwa kutoka kwa nywele zake, ao kufanyiwa unyanyasaji wa aina yoyote.
- Finlande ina fasi mzuri kwa masomo ya watoto wadogo, na watoto wote kati ya miaka 7 na 17 wanahuzuria masomo ya msingi na sekondari. Upatikanaji wa shule na masomo ya utotoni umehakikishiwa na sheria.

# Kuwa Finlande kama mhamiaji

**Katika Finlande, wahamiaji walio na haki ya kisheria, kama sehemu ya wakimbizi wanaohamia inchi ya tatu, ni washirika kamili wa jamii na wana haki na madaraka sawa ya kiraia kama wakaazi wengine inchini Finlande.**

1. Ili kufanya zoezi hili, unaweza kutembelea ukurasa wa site kupitia kiungo ao alama wa QR Sehemu ya ukurasa huu wa site imejumuishwa, lakini maandishi kamili yanapatikana tu kwa ukurasa wa site.

   Hebu tusome maandishi:
   infofinland.fi/en/living-in-finland/settling-in-finland/your-rights-and-obligations-in-finland

---

Kila mtu ana haki ya kutendewa sawa. Hakuna mtu anayepaswa kutendewa tofauti kwa msingi wa jinsia, umri, dini au ulemavu, kwa mfano. Kila mtu ana haki ya kueleza maoni yake kwa maneno ao kwa maandishi. Hakuna mtu anayeweza kuhukumiwa kifo ao kuteswa. Kila mtu ana haki ya kulindwa kuhusiana na mambo zake ya upeke. Kila mtu yuko huru kuchagua dini yake mwenyewe. Ikiwa hautaki, hauhitajiki kuchagua dini yoyote.

Wageni wanaoishi kwa kudumu inchini Finlande ambao wana zaidi ya miaka 18, wana haki ya kupiga kura katika uchaguzi za miji. Wageni ambao wana haki ya kupiga kura katika uchaguzi za miji pia wana haki ya kugombea viti katika uchaguzi za miji. Watu wote wanaokaa au wanaoishi Finlande lazima wafuate sheria za Finlande.

Shule ya lazima (oppivelvollisuus) ina masomo ya mbele ya shule ya msingi ya mwaka moja kwa watoto wa miaka 6 na masomo ya msingi ya miaka tisa kwa watoto wenye umri wa miaka 7-16, yaani, lazima wakamilishe programme ya shule ya jumla (peruskoulu). Wazazi wana jukumu la kuwatunza watoto wao. Kila mtu ana madaraka ya kutoa msaada wake ajali inapotokea.

---

Sasa kwa kuwa umesoma maandishi, hebu tusome maulizo na tuyajibu.

**a.** Je, wahamiaji wote wanaweza kupiga kura na kugombea uchaguzi za miji?

**b.** Je, una madaraka wa kuwa na dini inchini Finlande?

**c.** Je, masomo ya lazima hudumu miaka sita?

**d.** Je, gazabu ya kifo inaruhusiwa?

**e.** Je, haki za kujieleza na za kidini katika Finlande zinamaanisha kuwa jamii za Waislamu zinaweza kutumia sheria za Kiislamu kuliko sheria ya Finlande?

!

- Katika Finlande, unaweza kufanya ginsi unavyopenda na kipeke kile unachotaka ila tu unaheshimu sheria.
- Katika Finlande, unaweza kuwa na uaminifu kwa mamlaka.
- Katika Finlande, kila mtu ana haki na madaraka sawa.
- Kila mtu ni sawa, na watu wanaheshimiana na kusaidiana.

2. Hatua ya kuingia katika jamii inavyofaa na jamii ya Finlande inahitaji juhudi katika kujifunza luga ya wenyeji. Karibu asilimia 90 ya watu wa Finlande wanazungumza Kifinalnde kama luga yao ya asili. Utahitaji uwezo ya kujua luga ya Kifini au Kiswidi katika masomo, kazini na maisha ya kila siku. Ginsi unavyojifunza kwa haraka siri wa kimsingi katika luga ya wenyeji, ndivyo unavyojiingisha kwa namna ya haraka katika jamii ya Finlande. Angalia salamu na maneno ya msingi katika Kifinlande kwa mwisho ya kitabu hiki cha kazi!

   Hebu tusome zaidi kuhusu luga hizi mbili za kitaifa:
   infofinland.fi/en/living-in-finland/finnish-and-swedish/why-should-i-study-finnish-or-swedish

Hebu tusome maulizo na tuyajibu.

- **a.** Je, luga mbili za kitaifa za Finlande ni gani?

  ______________________________

- **b.** Ikiwa unataka kusoma ao kufanya kazi inchini Finlande, unapaswa kufanya nini kwanza?

  ______________________________

  ______________________________

- **c.** Kuna faida gani mengine ikiwa utajifunza luga ya wenyeji?

  ______________________________

  ______________________________

- **d.** Je, kujua wa luga za Kifinland au Uswidi ni sharti la kupata uraia wa Finlande?

  ______________________________

**e.** Kazi ya kuongeza: Angalia tangamano chache muhimu katika Kifinlande na ujaribu kuzisema:
infofinland.fi/en/living-in-finland/finnish-and-swedish/important-sentences-in-finnish

!

- Kujiingiza unahitaji juhudi: Una mapashwa la kibinafsi la kujifunza luga na kutafuta na fasi.
- Mtazamo wa watu wa Finlande kwa wahamiaji kawaida ni wa kirafiki.
- Ubaguzi umepigwa marufuku na sheria inchini Finlande.

Sasa kwa kuwa umemaliza sehemu, acha tufupishe kwa kuandika mawazo muhimu ambayo umejifunza kuhusu kila jambo iliyotajwa hapo chini!




- Finlande itakuwa nyumbani mpya kwako. Jinsi unavyofahamu maelezo zaidi, ndivyo ni bora. Acha tuchukue kwa umuhimu kujifunza Kifinlande na tuulize maulizo wakati wowote inahitajika.

# Majibu

## Eneo la kijiografia na idadi ya watu

1. Estonia | Urusi | Uswidi | Ufaransa | Ujerumani | Kanada | Norwe

2. Ulaya

3. Pahali pa Finlande kwa ramani ni pafuatayo.



4. Majibu yanatofautiana; uliza mwalimu wako ao utumie mtambo wa kutafuta.

5. Majibu yanatofautiana kulingana na historia yako ya kibinafsi.

## Hali ya hewa

1. Picha ambazo hazijapigwa Finlande ni pamoja na: b, g, I, m, na o.

2. Majibu yanatofautiana, hata hivyo utahitaji kujiandaa vizuri kwa ajili ya baridi. Katika wakati tofauti unaweza kuwa na shuruli tofauti za inje, kama vile kuogelea wakati wa kipwa na kucheza ski wakati wa baridi. Katika wakati wa baridi, halijoto ya inje inaweza kuwa ya chini, lakini kutokana na chombo ya kupasha joto inayopatikana katika nyumba zote, mazingira ya ndani yana joto kwa mwaka mzima, na maisha kamili yanawezekana wakati wowote.

## Majimbo na miji

**1.** Ramani iliyo na majina na alama ya majimbo inaweza kuonekana hapo chini.



## Njia kubwa ya kupata vyakula

**1.** Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| | | |
|---|---|---|
| a. | Hapana | Katika inchi za Kaskazini, ni Finlande na Aisilandi pekee ndizo jamhuri. Uswidi, Denmarki na Norwe ni falme. |
| b. | Ndiyo | |
| c. | Ndiyo | Vifaa ya kiektroniki, kemikali, na mashine nzito ni mauzo muhimu ya inje pia. |
| d. | Hapana | Hapo zamani, misitu zilitoa chakula kwa watu wa Finland wengi, hata hivyo siku hizi tangu kilimo kiwe cha kimitambo, misitu zinatoa kazi kwa hesabu ndogo tu. |
| e. | Ndiyo | Watu wa Finland wengi wanafanya kazi katika uwanja wa kiteknolojia na kampuni nyingi za Finlande zinahusika katika sekta za teknolojia na utumishi. Kampuni inayojulikana ya simu ya Nokia ilianza Finlande, na jina la kampuni hiyo linarejelea mji wa Nokia; unapaswa kuutembelea! |
| f | Hapana | Mnamo 2017 hesabu ya watu ilikuwa milioni 5.5. Angalia ni watu wangapi wanaoishi Finlande kwa kutembelea site ya Shirika la Utumishi Dijitali na Data ya Hesabu ya Watu kwa dvv.fi. |
| g. | Ndiyo | Jina la Finlande katika luga ya Kifinlande ni Suomi. |
| h | Hapana | Luga za Kifinlande na Kiswidi tu ndio rasmi, na Kifini ndiyo luga inayotumiwa zaidi inchini. |
| i | Ndiyo | Unaamini hii? Soma kuhusu hii katika Wikipedia kwa kutembelea kiungo kifuatacho en.wikipedia.org/wiki/Swamp_football. |

## Mazoea ya kitamaduni

**1.** Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| a. | b. | c. | d. | e. |
|---|---|---|---|---|
| kutikisa kichwa | kwa uangalifu | ujeuri | ahadi | wikendi |

**Ulizo la kuongeza:** Uongo. Siku ya Uhuru ya Finlande ni tarehe 6 Septemba.

## Nafasi za wanamemba ya jamaa

**1.** Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| a. | b. | c. | d. | e. | f |
|---|---|---|---|---|---|
| x | z | v | u | w | y |

**Ulizo la kuongeza:** 1906

## Kuwa Finlande kama mhamiaji

**1.** Majibu ya maulizo kwenye ukurasa wa 20–21

| | |
|---|---|
| a. | Ikiwa hautaki, hauhitajiki kuchagua dini yoyote.Wageni wanaoishi kwa kudumu inchini Finlande ambao wana zaidi ya miaka 18, wana haki ya kupiga kura katika uchaguzi za miji. |
| b. | Kila mtu yuko huru kuchagua dini yake mwenyewe. Ikiwa hautaki, hauitaji kuchagua dini yoyote. |
| c. | Masomo ya lazima ni kwa watu wenye umri wa miaka 6-16. |
| d. | Hakuna mtu anayeweza kuhukumiwa kifo ao kuteswa. |
| e. | Jamii za kidini, ikiwa ni pamoja na Wakristo, Wayahudi, Waislamu, Wahindu, na wengine wako huru kufuata dini yao, lakini lazima wafuate sheria za Finlande. Katika Finlande, sheria za Finlande zinachukua nafasi ya sheria yoyote ya kidini. |

**2.** Majibu ya maulizo kwenye ukurasa wa 22:

| | |
|---|---|
| a. | Kifinlande na Kiswidi |
| b. | Jifunze luga |
| c. | Kufuatilia maisha ya kila siku na kuunda urafiki na watu wa Finlande |
| d. | Ndiyo |

# Kujiandaa

**Kujitayarisha – Kujitayarisha Kwa Kuishi kwa Finlande**



Kabla ya kuondoka, matayarisho fulani yanahitajika kufanywa.

Mbali na mizigo yako, lazima ujiandae kiakili kwa safari yako.

**Katika sehemu hii, utajifunza kuhusu:**

- Kujiandaa kwa Uhamiaji wa Kudumu
- Mambo gani muhimu ya kuendelea kufuatilia
- Jinsi ya kujiandaa kwa kujiingiza kwako katika jamii
- Mshtuko wa kitamaduni ni nini na jinsi ya kuvitana naye

**Soma kuhusu sehemu hii katika mof.fi/sections/preparing/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

**Pata sehemu hii mtandaoni katika mof.fi/exercises/preparing/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

# Kujitayarisha kwa kuhama kabisa

Hebu tusome maandishi:

---

Kama mkimbizi anayehamia inchi ingine na wale walioongezwa kwa faili (dossier) yako uliyoleta wamepewa hali ya ukimbizi, vibali vya kuhamishwa vinavyoendelea, na haki ya kufanya kazi nchini Finlande. Ni muhimu kuzungumuza na wanamemba ya jamaa yako kuhusu matarajio ya uhamiaji wa kudumu na maana yake, na ni vizuri kujitayarisha kwa safari hiyo mkiwa pamoja. Mbele yako kuna mazingira mapya ya kuishi na watu wapya wenye mila na desturi tofauti, na ambao watazungumza nawe kwa luga mpya.

---

Zungumuzia hili pamoja na jamaa yako ao wenzako. Ikiwa mwanamemba mumoja ya jamaai kuandika, unaweza pia kumusaidia.

**1.** Unapohamia Finlande, unataka kufikia malengo gani? Je, unapanga kulea jamaa? Kupata makuta? Kuwa na utulivu na amani ya akili? Kuhakikisha na fasi za masomo kwa wewe ao kwa jamaa yako? Kitu ingine?

______________________________

______________________________

______________________________

**2.** Je, uko tayari kufanya nini ili kufikia malengo haya? Je, uko tayari kujifunza luga ya kigeni? Je, uko tayari kujitoa ili kuingia katika jamii mpya? Kitu ingine?

______________________________

______________________________

______________________________

!

- Kupata fasi mpya ya kuishi kwa Finlande ni mwanzo ya hatua mpya katika maisha. Jikazefaida kufanya maisha yako mapya kuwa mazuri na yenye manufaa.

**3.** Kulingana na majibu yako hapo juu, andika barua kwa rafiki yako ao mwanamemba ya jamaa inayoelezea kwa nini unataka kwenda Finlande, nini utafanya huko, na nini ambacho uko tayari kufanya ili kufanikiwa. Ongeza maelezo mengi kama inawezekana.



- Watu wanabadilikaga, na wewe hauko tofauti. Unaweza kutembelea site kabla na baada ya kupata pahali pako mpya katika Finlande. Wakati fulani, unaweza kuhisi upeke na kusahau sababu zilizokufanya ufanye maamuzi fulani; barua hii inaweza kukusaidia ukumbuke sababu chache.

# Barua za usafiri na vyeti vingine

Ukurasa wa somo, ambao unapatikana kupitia kiungo kinachopatikana kwa mwanzo ya sura hii, kuna maelezo kuhusu hati za usafiri, vyeti vya shule na kazi, pamoja na dawa zilizoandikwa na munganga. Inayofuata hapa chini ni tu sehemu ndogo ya ile ukurasa. Hebu tuzisome.

---

Kumbuka kwenda na barua zote za usafiri na barua za utambulisho. Hati halisi husaidia katika mchakato wa usajili, na baadaye, katika kupata hati mpya za usafiri.

Ni muhimu kwenda na vyeti vyote halisi vinavyohusiana na masomo na kazi. Ni vizuri kuthibitisha vyeti kwa kutumia mthibitishaji na, ikiwezekana, kuzitafsiri kwa Kizungu tayari katika nchi unayoondoka.

Katika mahojiano ya kwanza katika kituo cha afya, muuguzi wa afya ya umma atapitia historia ya maradhi, dawa, na chanjo zako za awali. Kwa hivyo, ni muhimu kwenda na maagizo ya zamani, taarifa za madaktari, na kadi za chanjo kutoka nchi unayoondoka. Hizi zitasaidia kuharakisha mchakato wa kupata matibabu na dawa sahihi katika manispaa yako mpya ya makazi. Unapaswa pia kwenda na dawa zako za lazima za mwezi mzima.

---

**1.** Sasa kwa kuwa umesoma maandishi, je, unadhani una kitu kinacholingana ambacho unapanga kwenda nacho kutoka eneo lako la sasa? Hebu tutumie orodha hapo chini kama kikumbusho muhimu. Weka alama kwa vitu ambavyo utabeba na uandike vitu vingine vinavyofanana na ya muhimu.

| **Kitu** | ☐ | **Maelezo** |
|---|---|---|
| Barua ya usafiri | ☒ | |
| Vyeti vya shule | ☐ | |
| Vyeti vya kazi | ☐ | |
| Dawa | ☐ | |
| Vyeti vya matunzo | ☐ | |
| Picha ya jamaa | ☐ | |
| Barua zingine za kibinafsi | ☐ | |
| | ☐ | |
| | ☐ | |
| | ☐ | |

**!**

- Barua zinazohusu historia yako ya matunzo na historia yako ya masomo na kazi, na pia barua zingine rasmi ni muhimu sana. Hakikisha kuwa unakwenda nazo.

# Mpango wa masomo na kutafuta kazi

Baada ya kufika katika muji ya nyumbani, utaanza mpango wako wa kuingia ndani ya jamii. Hebu tusome maandishi na tujibu maulizo ili kujua zaidi kuhusu haya.

Ili kufanya kazi inchini Finlande, wahamiaji kawaida wanahitaji kupitia majifunzo ya kuingia ndani ya jamii na kupata masomo zaidi inchini Finlande. Ili kuhakikisha unapata masomo inayofaa inchini Finlande, unapaswa kufanya mpango mbele ya masomo na zaidi ufanye kazi tayari katika pahali pako ya sasa. Katika mpango yako unapaswa kuongeza wapi, namna gani, na nini umesomea, diplomes gani umepata, na wapi umefanya kazi. Unapaswa pia kuandika ile kitu unajua kufanya vizuri na zawadi yako ya kibinafsi kuhusiana na aina ya kazi ambayo itakufaa. Pia ni muhimu sana kueleza mambo yale unaweza kufanya vizuri na ile umefanya tayari. Unaweza kupata namna ya kufanya kuhusu ginsi ya kuandika ile toka kwa wafundi kwa internet.

**1.** Je, unaamini uko tayari kupata masomo zaidi nchini Finlande? Kwa nini?

**2.** Je, kwa mpango wako utaongeza nini? Soma maulizo kutoka kwa maandishi na uyajibu.

**3.** Andika aina ya ile unajua kufanya na aina ya kazi unayoamini itakufaa.

Mara tu baada ya kuhamia Finlande, watoto wanawekwa katika madarasa ya maandalizi kwa watoto wahamiaji ambayo huwatayarisha kwa masomo ya jumla. Ni muhimu kwamba wazazi watayrishe watoto wao kuvitana na mazingira mapya ya masomo. Unaweza kupata maelezo kuhusu namna masomo inatumika kwa Finlande kupitia sehemu ya luga na viungo kwa site ya mof.fi.

**4.** Je, umezungumuza na jamaa yako kuhusu mpango wa kila mtu, ikiwa ni pamoja na watoto wako? Mumezungumuzia nini?

**5.** Angalia sehemu ya viungo kwa site ya Kuhamia Finlande.

!

- Kila mtu atakuwa na mpango wake wa masomo na kazi.
- Mpango wako mwenyewe ni ramani yako ya kufaulu inchini Finlande.
- Anza kufikilia kuhusu malengo unayotarajia kufikia.

# Matayarisho ya kiakili kwa ajili ya kuhama

**1.** Je, unatarajia kupata faida kwa Finlande? Una woga ya kupoteza nini? Katika zoezi ya kufuata, kuna mambo fulani ambazo zinaweza kukuhusu. Uzisome na uzipange katika vitu unavyotarajia kupata, mambo uanyoogopa kupoteza, ao mambo ambazo unafikili hazitabadilika ao hazikuvutii.

Marafiki

Amani ya kiakili

Mabadiliko katika tabia ya kila siku

Kujifunza luga

Kuunda upya jamaa inchini Finlande

Utamaduni mpya

Uhuru wa kidini

Mawasiliano na jamaa nyumbani ao inchi ya sasa

Kazi

Kusahau luga

Hali ya hewa

Nguvu

Utumishi za afya

Utajiri

| ☺ **Matumaini** | ☹ **Woga** | 😐 **Hakuna mabadiliko** |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

**2.** Ongeza vitu vingine utakazofikilia, ziwe ni za kukufaidia, kupoteza, au kubaki kama vilivyo.

**3.** Je, una maoni gani kuhusu ubao? Je, unaona kana kwamba kuna woga zaidi ao matumaini zaidi?
Weka alama ya mviringo kwa matumaini muhimu zaidi na woga mbaya zaidi uliyonayo.

______________________________

______________________________

______________________________

**4.** Je, unazani uko tayari kwa mabadiliko yatakayotokea katika mazingira yako ya kuishi? Je, unaona faida ya mabadiliko haya? Unafikili utapitia mabadiliko ya aina gani kisha ya kuhama kwaFinlande?

______________________________

______________________________

______________________________

# Kuzoea utamaduni mpya

**Kwa Finlande, wanawake na wanaume, vijana kwa wazee, wahamiaji na watu wa Finlande, wanachukuliwa kuwa sawa.**

Katika kurasa zifuatazo, kuna picha mbalimbali za watu. Hebu tutazame picha kwanza na kisha tusome maulizo.

**1.** Je, wanawake na wanaume wanafanya nini kwa picha?

**2.** Je, una maoni gani kuhusu picha ya "a" na "b"?

**3.** Je, kuna picha ambazo zinaweza kukuonyesha? Kwa nini?

**4.** Je, kuna picha ambazo hazikuonyeshe? Kwa sababu gani?

**5.** Pata picha ambazo zinaonyesha kila moja ya taarifa zifuatazo kulingana na maoni yako.

**a.** Jamaa inaweza kuwa mwanamume na mwanamke..

**b.** Jamaa inaweza kuwa na mzazi mumoja.

**c.** Jamaa inaweza kuwa watu wawili wa jinsia moja.

**d.** Wanawake wanaweza kufanya kila aina ya kazi.

**e.** Wanaume hufanya kazi za nyumbani na kutunza watoto.

**f.** Wanaume wanaweza kufanya kila aina ya kazi.

**g.** Watu wanaweza kueleza maoni yao kwa uhuru.

**h.** Pia kuna watu wasio na nyumba na ni masikini inchini Finlande.

**i.** Wazee na vijana inchini Finlande wanaweza kufurahia maisha.

**j.** Wageni na watu wa Finlande, wanaume na wanawake wanafanya kazi pamoja katika nafasi moja.

**k.** Kila mtu, bila kujali umri na jinsia, ana haki ya kuchagua mavazi yake na anachofanya ila tu anafanya hivyo ndani ya mipaka ya sheria.

**l.** Uhuru wa kidini unaheshimiwa.

**mM**. Mtu yeyote anaweza kucheza spoti inchini Finlande.

**n.** Pia kuna watu wenye ulemavu inchini Finlande.

**6.** Ikiwa unakutana na mtu ambaye hakubaliani na maoni yako ya kidini ao ya kisiasa, unaweza kufanya nini?

**7.** Kama mgeni inchini Finlande utakuwa kwa sehemu ya wachache. Je, una maoni gani kuhusu hii? Je, utafanya juhudi gani kuingiliana na watu wa Finlande?
Je, utafanya juhudi gani kuingiliana na vikundi vingine?

**!**

- Usawa ni moja ya faida muhimu zaidi katika jamii ya Finlande.
- Ubaguzi wa kijinsia, asili, dini, mwelekeo wa kijinsia, ao sababu ingine yoyote, imekatazwa na sheria.


a


b


c


d


e




f



g


h


i


j


k


l


m


n


o


p


q


r


s


t

- Wanawake na wanaume wanashiriki kwa kiwango sawa katika mambo yote ya maisha.
- Wanawake wa kila umri wana jukumu kamili inje ya nyumba. Inaweza kuhusiana na burudani, masomo, kazi ao kitu kingine chochote. Wanawake na jamaa zao wanapaswa kujiandaa kwa madaraka mapya.

8. Soma taarifa zifuatazo na uandike ikiwa unakubaliana nazo ao hapana? Eleza kwa nini.

**a.** Unyanyasaji wa kijinsia ni kosa.

**b.** Kuvaa nguo fupi haimaanishi kuwa wanawake wanaweza kunyanyaswa.

**c.** Unyanyasaji kwa nyumba unaweza kutokea katika kila aina ya familia - matajiri, walio na masomo, na masikini.

**d.** Wanawake wanachangia katika uchumi wanapofanya kazi inje ya nyumba.

**e.** Tamaduni au dini fulani tu ndizo zinazonyanyasa wanawake.

!

- Wanawake na wanaume ni sawa.
- Wanawake wana haki ya kufanya kazi, kusoma, na kuishi maisha huru.
- Unyanyasaji wa kijinsia ni kosa kila wakati.
- Vurugu daima ni kosa.
- Hakuna mtu - ikiwa ni pamoja na jamaa - anayeweza kuazibiwa kutokana na chaguo yake ya maisha, ikiwa anafuata sheria za Finlande

**9.** Hebu tuangalie kazi zifuatazo na tuzisome. Zungumuzia kuhusu ni nani anafanya kila kazi katika jamii yako ao katika jamaa yako? Sasa andika kwa ubao ni nani unafikili anafanya kazi hiziinchini Finlande.

Kupika

Kusafisha

Kubadilisha nepi

Kulipa kodi

Kurekebisha vifaa vilivyovunjika

Kunywa pombe

Kutengeneza kahawa

Kufanya kazi inje nyumba

Kuchukua watoto kutoka masomo

Kuanzisha biashara ya jamaa

Kufanya kazi kama munganga

Kufanya kazi kama msaidizi wa nyumba

| Wanaume | Wanawake |
| --- | --- |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |


**!**

- Nchini Finlande, wanaume na wanawake wanakuwa na madaraka ndani na inje ya nyumba.
- Kuwa na mawazo wazi; kuwa tayari kufanya mambo mengi ambayo hukuweza kufanya, na mambo mengi ambayo haukuwa tayari kufanya.

**10.** Je, unatumia sana mkono wa kushoto ao wa kuume? Ikiwa unatumia sana mkono wa kuume, weka kalamu mkononi mwako wa kushoto, na ikiwa unatumia sana mkono wa kushoto, weka kalamu kwa mkono wako wa kuume.

Kwa kila pahali pa maandishi hapa chini, andika tangamano moja mara tatu. Unaweza kuandika tangamana ya Kizungu "I can write." ao tangamano ya Kifinlande "Minä osaan kirjoittaa.". Unaweza pia kuchagua kifungu cha maneno ukitumia alfabeti ambayo unaifahamu zaidi. Ikiwa huwezi kuandika, chora nyuso tatu zile zinafurahi, ☺☺☺, kwa kila karatasi.

Sasa chagua tangamano na uiandike mara tatu kwa kila karatasi, kwa hivyo mara kumi na tano kwa jumla.



Hiyo haikuwa ngumu sana, sivyo?


Kumbuka ginsi unajisikia, kwa sababu **hivyo ndivyo kujifunza Kifinlande na kuingia katika jamii ya Kifinlande inakuwa mara ya kwanza.**. Kama ulivyotambua, ilichukua muda mrefu lakini uliweza kuifanya. Kujisikia hiyo ya kufanikiwa ndio utajisikia mara tu utakapofanikiwa kuwa na mazungumzo yako ya kwanza kwa Kifinlande: Kujisikia ya kupendeza.

**!**

- Kuingia katika jami ni hatua mrefu na kujitayarisha kiakili ni muhimu.
- Jambo muhimu kwa kuingia kwako katika jamii ni kujua luga ya KiKifnlandefini, kuwa na mawazo wazi, na kuwa na utayari wa kujifunza mambo mapya.

Katika zoezi hili, utasoma kuhusu mshtuko wa kitamaduni na jinsi ya kuvitana naye.

**Je, mshtuko wa kitamaduni ni nini? Mshtuko wa kitamaduni ni mafazaiko yanayosababishwa na ugumu wa kuelewa jinsi utamaduni mpya unavyofanya kazi. Sio kila mtu anayepitia mshtuko wa kitamaduni, lakini ni vizuri kujua ni nini na ginsi ya kuviatana naye, ikiwa utaupitia.**




**Kazi ya kuongeza!** Unaweza kusoma zaidi kuhusu mshtuko wa kitamaduni kwa Wikipedia katika en.wikipedia.org/wiki/Culture_shock ao kwa kusoma alama wa QR.

**11.** Kwa grafu, unaweza kusoma majina ya hatua ine za mshtuko wa kitamaduni. Hapo chini, utapata maelezo mafupi ya hatua hizi.
Sasa hebu tusome maelezo na tulinganishe kila moja na hatua ya kufaa.

| | |
|---|---|
| **a.** Wakati muzuri kisha arusi | **w.** Umefika kwa kiwango ya kufahamu zaidi kuhusu ginsi ya kushurulikia utamaduni na kuanza kuzoea utamaduni kwa mtazamo mzuri. |
| **b.** Kuchanganyikiwa | **x.** Unaweza kushiriki kikamilifu katika utamaduni mpya. Bado unaendelea na sehemu za utamaduni zako za zamani lakini pia unajifunza mambo mengi mapya kuhusu utamaduni yako mpya na kuhusu wewe mwenyewe pia, na unatimiza tamaduni nyingi kwa njia ya kibinafsi. |
| **c.** Marekebisho | **y.** Vitu vingine vinaweza kuonekana kuwa tofauti na utamaduni yako na unaweza kujisikia mwenye wamemukosea ao kuviona kuwa vya kushangaza, labda kusababisha kujisikia za furaha kubadilika na kuwa kujisikia za kukata tamaa na kutokuwa na furaha. Kwa Finlande, hii inaweza kutokea unapovumbua kuwa watu kila wakati wanataka kulinda nafasi zao za kibinafsi ao kwamba Kifinlande ni nguvu kujifunza. |
| d. Kukubalikana mambo mapya | **z.Z.** Kwa mwanzo, watu wengi wanafurahi kuhusu utamaduni mpya na wana hamu ya kuvumbua mambo na kuanza kuzungumza na watu. |

**!**

- Mshtuko wa kitamaduni ni mafazaiko yanayotokana na kutoweza kuelewa ginsi mazingira mapya yanavyofanya kazi.
- Unaweza kuchunga mshtuko wako wa kitamaduni na uingie vizuri.

**Sana, watoto wake na kakake Sam walihamia Finlande kwa 2015 kama wakimbizi. Baada ya kuhamia Finlande, Sana na jamaa yake walipitia hatua mbalimbali za mshtuko wa kitamaduni. Sana ameendelea kuzungumuza na rafiki kutoka nyumbani na kumuelezaa kuhusu kile kilichokuwa kikiendelea katika maisha yake. Hebu tujaribu kuona kile yeye na jamaa yake wamekuwa wakipitia.**

Hebu tusome ujumbe wote ambao Sana alituma na kujibu maulizo baadaye.

Ujumbe wa "a"

9:41 Asubui 70 %

< Mazungumzo Mai

Jambo Mai! Huyu ni Sana! Hii ni namba yangu mpya ya Finlande. Nilifika salama Finlande! Pahali hapa ni pa ajabu.

Pasafi sana! Miti kila nafasi na hewa ni safi sana. Watu ni wazuri sana. Nyumba yangu bado haina vitu lakini inapendeza sana na duka kubwa iko dakika tano tu kutoka hapa!

Sasa niko kwa fasi ya kuchukua bus na chini ya dakika 10 nitakuwa katika duka kubwa la jiji.

Haya ndio ile inaonekana kutoka kwa fasi ya kuchukua bus.



Ninaipenda!

**12.** Je, Sana alikuwa akipitia hatua gani kwa ujumbe wa "a"?

Ujumbe wa "b”

10:41 Usiku 50 %

< Mazungumzo Mai

Mai, umekuwa wapi? Nakuhitaji. Nimekukosa sana. Nimekosa kila mtu. Ninalia kila wakati na ninafikilia kuhusu wakati mume wangu alipokuwa hai. Ninamukosa sana. Ninakosa shangazi Zina na jamaa yangu ya zamani.

Hakuna mtu anayezungumza nami hapa. Hali ya hewa, inanyesha daima ao kuna teluji. Watu wanashurulikia mambo yao na hawakuangalii wala kukusalimu. Kila wakati watoto wanakwenda kwa masomo ninawakosa sana. Ninaajua ni salama sana lakini bado ninawakosa sana na kuwaza juu yao.

Siku ya ine iliyopita niliaibika sana. Nilikwenda kwa duka kubwa na nikalipa makuta kadiri isiyofaa Sikuelewa kile alichokuwa akiniambia hadi mwanamume mumoja aliponielezea kwa Kizungu. Nilisikia haya sana. Kuanzia sasa nitatumia tu kadi yangu ya benki kwani inafanya mambo kuwa rahisi. Bado sina kazi. Huku lazima uzungumze Kifinlande hata kwa kazi ya kusafisha. Na Kifinlande ni nguvu na matata sana!

Ninakukosa rohoni.

**13.** Je, Sana alikuwa akipitia hatua gani kwa ujumbe wa "b"?

Ujumbe wa "c”

●●●○○ 06:55 Asubui 50 %

< Mazungumzo Mai

Mai, jamaa yako iko namna gani? Hatujazungumza kwa muda mrefu!

Mengi yametokea tangu wakati tulipozungumza. Nimekuwa na shuruli mingi, kuliko vile nilivyokuwa nyumbani. Nilimaliza somo yangu ya luga na nikaanza majifunzo ya kinganga. Mara moja kwa wiki bado ninahuzuria somo ya luga ya kibinafsi, na mara mbili kwa mwezi ninahuzuria tukio hili la kuingia katika jamii na wengine na kunywa kahawa.

Inaitwa kielikahvila kwa Kifinlande. Watu wengi wanaenda kule. Nilikutana na watu wa Finlande wengi kule. Nilikutana pia na wageni wengi.

Je, unajua kuwa jina la Finlande katika Kifinlande ni Suomi? Watu wa Finlande wanaita Finlande hivyo. Wanaiita Suomi. Kwa hivyo, hadi sasa nimekutana na watu kutoka Suomi, kutoka Argentina, kutoka Vietnamu, kutoka Israeli, kutoka Urusi, kutoka Algeria, kutoka Namibia, kutoka Tunisia na hata kutoka Austria. Wote wanataka kujifunza na kuzungumza Kifinlande na luga zingine.

Wakati mwingine ninafanya kazi na kampuni inayohitaji watu wanaozungumza luga yetu. Niliunda kitu hiki cha kazi kinachoitwa toiminimi na ni kama kuwa na kampuni yangu mwenyewe. Inanisaidia kupata kazi wakati mwingine.

Watoto je! Unajua kwamba wanazungumza Kifinlande bora kuliko mimi! Ninazungumza Kifinlande ya katikati sasa, lakini watoto ni zaidi! Unapaswa kuwasikiliza wakizungumza tunapokutana na waalimu. Unaweza kuzani ni wazaliwa wa hapa.

Nimepata marafiki zaidi sasa na ninajaribu kwa utaratibu kutengeneza vizuri Kifinlande changu. Hii ndio jambo muhimu zaidi. Endelea kuzungumza nami, Mai! Nimekukosa sana.

**14.** Je, Sana alikuwa akipitia hatua gani kwenye ujumbe wa "c"?

Ujumbe wa "d"

●●●○○ 07:01 Asubui 50 %

< Mazungumzo Mai

Mambo sio sawa kati yangu na Sam, haendi kwa masomo yake ya luga na nimejulishwa kuwa atavitana na hatari nyingi ikiwa ataendelea hivi.

Nilimwambia kuwa anapoteza mwelekeo wa maisha yake. Inchi hii imempa nafasi na anaipoteza hivyo tu.

Wanaume wengine waliokuja nasi mwaka hii tayari wana kazi ao tayari wanasoma ili kufikia malengo yao lakini yeye hata hajakamilisha somo ya luga.

Yeye ni kaka yangu, lakini nimepitia mambo yale yale ambayo amekuwa akipitia na watoto wangu na sasa ninazungumza nusu ya Kifinland na ninatarajia hivi karibuni nitaanza majifunzo yangu. Bado hawezi kuzungumza Kifinlande na hataki hata kujaribu!

Anasema anawachukia watu wa Finlande, lakini hata hawezi kuzungumza nao... Na anawalaumu kwa nini? Sababu ya kumpa kimbilio? Kumpatia somo ya luga bure? Utumishi ya bure ya afya? Anajaribu kuwalaumu kwa kosa lake yeye mwenyewe.

Nilijaribu kuzungumza naye, lakini haionekani kufanya kazi. Nilijaribu hata kumfundisha maneno fulani ya Kifinlande na kusoma pamoja naye lakini hataki na anakasirika sana ninapomwambia kwamba anahitaji kujifunza.

Anachofanya ni kukaa na marafiki wengine kutoka nyumbani, na wakati hafanyi hivyo, anakuja hapa na kucheza na michezo ya watoto wangu na hanisaidii katika kazi za nyumbani ao chochote! Asingekuwa ndugu yangu nisingekuwa mvumilivu sana naye.

Nina wasiwasi sana juu yake!

**15.** Je, ni hatua gani Sam alikuwa akipitia kwenye ujumbe wa "d"?

Ujumbe wa “e”

●●●○○ 21:12 Asubui 80 %

< Mazungumzo Mai

Hebu fikilia ni nani aliyeanza kazi yake rasmi ya kinganga?



Umepata! Mimi ni munganga kabisa sasa.

Tulihama kwenye nyumba mpya katika mji mdogo karibu na hospitali ambapo nilipata kazi hiyo.

Ninajaribu kupanga ginsi watoto watahamia masomo ingine.
Nina furaha kwamba namna ya kuendelesha masomo inchini Finlande inanipa namna ya kufuatilia ile watoto wanachojifunza.

Ninafikilia kununua gari. Tayari nimchunguza matangazo na kuzungumuza na watu katika Kifinlande. Nazani watu wengi wanafikili mimi ni mutu wa Finlande kwa sababu Sana linakaribia kufanana na jina la Kifnlande Sanna. Kwa kweli watu wengi wananiita Sanna kuliko Sana. Ilikuwa ya kushangaza kwa mwanzo lakini sasa hata mimi ninaitumia.

Unajua Kifinland ni nguvu lakini ni luga nzuri, na unaifurahia sana mara tu unapoizoea.

Nimekuwa pia nikiuzishaa sakafu fulani za kushuka! Unajua kama zile ambazo tulikuwa tukitengeneza nyumbani, lakini sasa ninatengeza kwa rangi za Finlande. Watu wanaonekana kuzipenda.

Ijapokuwa ninaziuza mtandaoni, lazima nifahamishe ofisi ya ushuru.

Ushuru ni muhimu sana hapa. Sasa ninajua jinsi ya kufikisha taarifa yangu ya ushuru kwa mwisho. Kwa kweli sio ngumu sana.

Na baada ya yote, ushuru wa watu wengine ulinisaidia kusoma na kuwa vile nilivyo leo, kwa hivyo ni sawa tu.

Kwa sasa, nitaendelea kufanya kazi na kufurahia ile maisha inanipa.

Ninajisikia vizuri.

**16.** Je, Sana alikuwa akipitia hatua gani kwa ujumbe wa "e"?

**17.** Je, unafikili Sana ameingia vizuri katika jamii ya Finlande?

______________________________

______________________________

______________________________

**18.** Je, ungefanya kitu tofauti ikiwa ungekuwa yeye?

______________________________

______________________________

______________________________

**19.** Kulingana na kile umesoma, ni ushauri gani utampa mtu ambaye anahamia kwa kutumika katika inchi ingine?

______________________________

______________________________

______________________________

!

- Una madaraka ya kibinafsi kuhusu kuingia kwako inchini Finlande.
- Kwa kujifunza Kifinlande, nafasi zaidi za kazi na burudani zitapatikana.

# Majibu

## Kujitayarisha kwa kuhama kabisa

1. Majibu yanatofautishana kulingana na malengo yako ya kibinafsi.
2. Kuweka mawazo wazi kuhusu ginsi ya kufikia malengo yako ni lazima. Mbali na kujifunza Kifinlande, utajifunza mambo mengine mengi. Kuwa tayari kwa safari yenye mafanikio.
3. Majibu yanatofautishana.

## Barua za usafiri na vyeti vingine

1. Hata hivi, lazima ukumbuke kuwa barua za usafiri, vyeti, na dawa ni muhimu. Ikiwa huna barua ya usafiri, utapewa moja.

## Mpango wa masomo na kutafuta kazi

1. Unapaswa kuwa tayari kupata masomo zaidi inchini Finlande. Utahitaji kujifunza Kifinlande na hata utahitaji kupata kujua mambo mapya.
2. Majibu yanatofautishana.
3. Majibu yanatofautishana. Unapaswa hata hivikuwa na mawazo wazi kuhusu aina gani ya kazi unayoweza kufanya.
4. Majibu yanatofautishana.

## Matayarisho ya kiakili kwa ajili ya kuhama

1. Majibu yanatofautishana kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi.
2. Majibu yanatofautishana kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi.
3. Majibu yanatofautishana kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi. Hata hivi, kuwa na mtazamo ulio na matumaini inaweza kukusaidia katika kujitayarisha vizuri kwa pahali pako mpya ya kuishi.
4. Majibu yanatofautishana. Kwa hali yoyote, kuwa tayari kubadilika na kujifunza mengi zaidi.

## Kuzoea utamaduni mpya

1. Majibu yanatofautishana. Kwa jumla, picha zinaonyesha watu tofauti kutoka Finlande na nafasi ingine wakifanya kazi ambazo wengi wanafanya katika Finlande.
2. Picha "a" inaonyesha kundi ya watu kutoka asili tofauti wanaofanya kazi pamoja. Picha "b" inaonyesha mwanamke kutoka asili ya wahamiaji anayefanya kazi.
3. Majibu yanatofautishana kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi. Kumbuka kwamba kila mtu yuko huru kujifananisha na picha chochote anayochagua.
4. Majibu yanatofautishana kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi. Kumbuka kwamba kila mtu yuko huru kutojifananisha na picha anayochagua.
5. Majibu yanaweza kupatikana kwenye ubao ifuatayo.

| **a** | **b** | **c** | **d** | **e** | **f** | **g** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| d \| h | i \| j | k | b \| m \| p \| t | i \| j | l \| s | f \| g |
| **h** | **i** | **j** | **k** | **l** | **m** | **n** |
| c | d \| n | a | c \| d \| e \| n | q | o | r |

6. Majibu yanatofautishana. Kumbuka kwamba imani za kibinafsi ni za kibinafsi tu.
7. Majibu yanatofautishana; unapaswa hata hivi kuwa na mtazamo mzuri kuhusu maisha yako inchini Finlande na utambue kuwa haki zako zimehakikishwa na sheria, na kwamba unahitaji kuingiliana na watu wa Finlande wengine na wakaaji wengine wa Finlande kwa ajili ya kujiingiza kwako katika jamii.
8. Majibu yanaweza kupatikana hapa chini.
   - **a.** Unyanyasaji wa kijinsia na ubakaji ni kosa na haupaswi kutokea kabisa.
   - **b.** Wanawake wako huru kuvaa na kufanya chochote wanachotaka chini ya mipaka ya kisheria. Kuvaa mavazi fulani haimaanishi mtu yeyote anataka kusumbuliwa.
   - **c.** Unyanyasaji wa kinyumbani haipatani na mapato. Unyanyasaji wa kinyumbani unaweza kutokea katika kila aina ya jamaa. Unyanyasaji wa kinyumbani daima ni kosa.
   - **d.** Wanawake wana haki ya kufaidika kutokana na kufanya kazi na kusaidia jamii pia. Hii pia inaleta ngivi na mapato zaidi kwa nyumba na watu walio chini yao, ikiwa mwenye anawasimamia atakufa ao hayuko tena, kwamba wanawake hawatalazimika kuwa wenye wanasimamia ao kutumia njia ambazo hawangetumia namna ingine.
   - **e.** Kuchokoza mwanamke inafika kila nafasi bila kujali utamaduni, dini, na kabila, ingawa ni tofauti kwa ginsi inavyoenea. Kutoka tamaduni ao asili fulani sio visingizio vya unyanyasaji ya wanawake, watoto ao watu wengine.
9. Majibu yanaweza kutofautishana kuhusu ni nani anayefanya nini katika jamaa yako, hata hivi kwa Finlande, mapashwa haya yote yanashirikishwa kati ya wanamemba ya jamaa bila kujali jinsia yao. Kumbuka kwamba kama mtu havunji sheria, ni kosa kumuzuia kufanya kitu ambacho anataka kufanya.
10. Hongera kwa kukamilisha zoezi. Unapaswa kuwa na mtazamo sawa inayohusu kuhama kwaFinlande.
11. Majibu yanaweza kupatikana kwa ubao ifuatayo.

| a | b | c | d |
|---|---|---|---|
| z | y | w | x |

12. Katika ujumbe wa "a", Sana alikuwa akipitia muda ya raha kisha arusi ya mshtuko wa kitamaduni.
13. Katika ujumbe wa "b", Sana alikuwa akipitia hatua ya kuchanganyikiwa ya mshtuko wa kitamaduni.
14. Katika ujumbe wa "c", Sana alikuwa akipitia hatua ya marekebisho ya utaratibu ya mshtuko wa kitamaduni.
15. Katika ujumbe wa "d", Sana alikuwa akipitia hatua ya kuchanganyikiwa ambayo inasababisha muda kamili ya kujitenga ya mshtuko wa kitamaduni.
16. Katika ujumbe wa "e", Sana alipitia kila hatua ya mshtuko wa kitamaduni na kwa hivi aliweza kufikia hatua ya kukubalika na mambo mapya, na kuweza kuchangia vizuri jamii yake.
17. Sana amejiingiza vizuri kwa Finlande na katika jamii ya Finlande.
18. Majibu yanatofautishana. Mfano wa Sana hata hivi ni mzuri sana.
19. Majibu yanatofautishana. Kumbuka kwamba kufikilia kusoma Kifinlande ndio ufunguo wa kujiingizza vizuri inchini Finlande.

# Kusafiri

**Kwenda Finlande**



Safari yako ya kwenda Finlande ni murefu; itakuchukua siku nyingi za kutayarisha na safari ya ndege hadi utakapofika kwa nyumba yako mpya. Kwa usaidizi wa maelezo kwa kurasa zifuatazo, safari itakuwa rahisi.

**Katika sehemu hii, utajifunza kuhusu:**

- Hatua za safari yako kwenda Finlande
- Nini kubeba na kutokubeba wakati wa kusafiri
- Nini kufanya kwa uwanja wa ndege
- Nini inatokea unapofika Finlande

**Soma kuhusu sehemu hii katika mof.fi/sections/travelling/en ao soma alama wa QR ulio hapa chini.**

**Pata sehemu hii mtandaoni katika mof.fi/exercises/travelling/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

# Kujitayarisha kwa safari ya ndege

**Safari ya kwenda Finlande itachukua muda na itabidi uchukue hatua mbalimbali hadi ufike kwa nyumba yako mpya katika muji yako mpya.**

**1.** Hebu tuangalie hatua zifuatazo na tuzipange kwa utaratibu.

mwaliko wa mahojiano na mamlaka ya Finlande | kuondoka | ukubali ya mamlaka ya Finlande |kufika kwa muji wapi nyumba yako mpya iko | kufika Finlande | mahojiano na mamlaka ya Finlande | kujitayarisha kwa safari ya ndege | majifunzo ya kitamaduni mbele ya kuondoka | kuanza kujifunza kuhusu utamaduni na luga mpya

Mwaliko wa mahojiano na mamlaka ya Finlande

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Kufika kwa muji wapi nyumba yako mpya iko

**2.** Je, umeelewa vizuri hatua za safari? Unatarajia safari itakuwa namna gani?

**Kazi ya kuongeza!**
Je, hatua kutoka wakati wa kupokea ukubali ya mamlaka ya Finlande hadi kusafiri kwenda Finlande kwa kawaida inachukua muda gani?

!

- Hautasafiri kwenda Finlande peke yako. Utapokea usaidizi wakati unaondoka, unapopita mipakani, na unapofika Finlande.

**3.** Soma na ukamilishe maandishi yafuatayo. Ikiwa unahitaji usaidizi, tumia maneno yanayopatikana hapa chini.



Shirika la Kimataifa la Uhamiaji

Safari ya kwenda Finlande inafanyika kwa ______________. Kuondoka ni toka Uwanja wa Ndege. Kwa sababu kila mtu ana ________________ tu kubeba kilo ________________ tu za mzigo, ni muhimu ________________ mbele ni vitu gani unataka kubeba na unachohitaji kuacha nyuma.

Wakati wa kwenda safari lazima ubebe barua za usafiri na tike za ndege. Ni muhimu pia kwenda na __________________ vya kibinafsi. Unahitaji kwenda na _____________________ yoyote ______________________ vingine vya nyumbani. Chakula au _________________________ haziruhusiwi kupita lango la __________________ la usalama.

vinywaji | vitu | kupanga | ndege | ruhusiwa | 20 | ukubali | vyeti | vifaa vya mapishi

**!**

- Safari yako itakuwa ndefu; ujitayarishe vizuri.
- Vitu vingi havihitaji kubebwa, fikilia kwa uangalifu kuhusu nini unapaswa kubeba na kutokubeba.

4. Unafikilia ni nini haitapatikane inchini Finlande na utahitaji kuibeba? Andika kwa sehemu ya maandishi hapa chini.

5. Hapa chini unapata maelezo na picha. Unganisha hali na aina ya mizigo.

- Kilo 20
- Zaidi ya lita moja ya vitu maji maji
- Inakaa na wasafiri wakati wa safari
- Kilo 8
- Kadiri ya juu ya vitu maji maji inayokubaliwa ni lita moja chini ya masharti fulani
- Haikai na abiria wakati wa safari

mzigo ya mkono




mizigo ya kawaida



- Kumbuka kuwa utakuwa na mzigo yako ya mkono tu, na hivi utarejeshewa mizigo yako mingine tu kwa Helsinki ao kwa eneo unayokwenda.

**6.** Hebu tuangalie picha zilizo hapa chini.
Weka alama ya x kwa vitu ambavyo huruhusiwi kusafiri nazo na haupaswi kwenda nazo katika uwanja wa ndege.
Vitu vilivyobaki vinaruhusiwa kupelekwa uwanja wa ndege. Weka alama ya mvirongo kwa vitu ambavyo unaweza kubeba kama mzigo ya mkono.




- Ni muhimu kwamba ubebe vyeti vyote halisi na vilivyotafsiriwa vinavyohusiana na masomo, diplome na kazi, barua za utambulisho na usafiri, pamoja na barua zinazohusiana na afya.

# Kwa uwanja wa ndege

**Kuna mambo mengi ya kufanya kabla ya kuingia kwa ndege. Kumbuka kufika kwa wakati kwa uwanja wa ndege!**

1. Kwa uwanja wa ndege, utapitia hatua nyingi mbele ya kuingia ndani ya ndege. Hebu tuunganishe picha na hatua inayolingana.
    - **a.** Kuingia
    - **b.** Kuzunguka uwanja wa ndege
    - **c.** Kuangalia pasipoti
    - **d.** Ukaguzi wa usalama
    - **e.** Kuingia kwa ndege

v



Shirika la Kimataifa la Uhamiaji

w




x



y



Shirika la Kimataifa la Uhamiaji

z



Shirika la Kimataifa la Uhamiaji

# Kufika

Hebu tusome maandishi.

Utafika Finlande kupitia uwanja wa ndege wa Helsinki-Vantaa. Kwanza itabidi uonyeshe barua zako za usafiri katika eneo la ukaguzi wa pasipoti. Utaleta barua kwa karani. Watu wanapitia ukaguzi wa pasipoti mumoja baada ya mwingine. Watoto wadogo zaidi wanaweza kuwa pamoja na wazazi wao.

Mamlaka ya Finlande itachukua maelezo ya kibinafsi, picha na alama za vidole unapofika Finlande ao mara tu baada ya kuandikwa kuwa umefika kwa Finlande. Hii inaweza kuchukua muda mrefu na unaweza kuulizwa ufungue masikio na shingo lako ikiwa una sakafu ili picha zako zipigwe.

Baada ya ukaguzi wa Pasipoti, kila mtu atakwenda kwa chumba kubwa wapi utasubiri mizigo yako uliyoacha kwa pahali pa ukaguzi ya inchi wapi ulioondoka. Mizigo zitafika kwa mikaba tofauti kulingana na safari ya ndege. Unaweza kuangalia safari ya ndege yako kutoka kwa ubao ya elektroniki. Ni muhimu kuhakikisha mizigo zote zimefika. Kuna vitu ya kusukuma mizigo kwa hiyo chuma wapi unaweza kuweka mizigo z ako. Mizigo zote zitakapofika utafuata mstari wa kijani kuelekea njia ya kutoka. Hii inamaanisha huna vitu za kutangaza. Basi utakuwa umeacha eneo la kimataifa na safari yako kwenda inchini Finlande inaweza kuanza.

Baada ya kuondoka katika eneo la kimataifa, utapata watu wa kujitoa wa Msalaba Mwekundu wa Finlande wakiwa wamevaa nguo ndogo nyekundu. Watu wa kujitoa watakusaidia katika kuendelea na safari yako. Kisha utaendelea na safari kwenda kwa muji wapi utaishi, ao kwa kutumia ndege ingine ao kupitia njia zingine za usafiri. Njia za usafiri zinapangwa kila wakati kwa ajili yako na utasaidiwa wakati wote wa safari.



Shirika la Kimataifa la Uhamiaji

**1.** Eleza picha iliyo hapa juu.

2. Ni gani ya kwanza? Kuchukua mzigo yako ao kupitia eneo la ukaguzi wa pasipoti?

3. Je, unaweza kuacha barua zako za kibinafsi kwenye mizigo yako iliyokaguliwa? Eleza kwa nini.

4. Kwa nini unaombwa ufungue masikio na shingo yako?

5. Je, ni aina gani ya vitu unapaswa kutangaza unaposafiri kwenda Finlande?

- Daima kuwa na barua zako za usafiri wakati wote! Shirikiana na mamlaka kwani itakusaidia na kila mtu mwingine aliye karibu nawe.

# Kisha ya kufika

1. Sasa kwa kuwa umefika katika pahali pako mpya, unaweza kupumzika na kisha muanze kujenga maisha yenu. Andika unachopanga kufanya mara tu kisha ya kufika Finlande.

- Safari ni ndefu na inachokesha. Ujitayarishe vizuri.
- Unapofika, maisha yako mapya yanaanza. Ni vizuri kufikilia kutulia na kujenga vizuri maisha yako inchini Finlande.

# Majibu





## Kujitayarisha kwa safari ya ndege

1. mwaliko wa mahojiano na mamlaka ya Finlande → mahojiano na mamlaka ya Finlande → ukubali wa mamlaka ya Finlande → kuanza kujifunza kuhusu utamaduni na luga mpya → majifunzo ya kitamaduni kabla ya kuondoka kujitayarisha kwa safari ya ndege → kuondoka → kufika Finlande → kufika kwa muji wapi utaishi
2. Majibu yanatofautishana, hata hivi unapaswa kujitayarisha kwa safari murefu.
3. ndege | kuruhusiwa | 20 | kupanga | vyeti | vifaa vya mapishi | vitu | vinywaji | ukubali

   **Swali la kuongeza:** Hatua kawaida inachukua hadi miezi sita.
4. Siku hizi, karibu vitu vyote za watumiaji zinaweza kupatikana katika duka za kawaida ao maalum kote Finlande. Hata hivi, kumbuka kubeba vitu vyako vya kibinafsi, kama vile dawa, dawa za maagizo na vyeti.
5. Ubao lililo hapa chini lina majibu ya zoezi.

| mzigo ya mkono | mzigo ya kawaida |
|---|---|
| • Kilo 8<br>• Kadiri ya juu ya vitu maji maji inayokubaliwa ni lita moja chini ya masharti fulani<br>• Inkaa na abiria wakati wa safari | • Kilo 20<br>• Zaidi ya lita moja ya vitu maji maji<br>• Haikai na abiria wakati wa safari |

6. Ubao lililo hapa chini lina majibu ya zoezi.

| a. Hairuhusiwi | b. Inaruhusiwa lakini haihitajiki | c. Inabebwa katika mzigo wa kawaida | d. Lazima ibebwe katika mzigo ya mkono | |
|---|---|---|---|---|
|  |  |  |  |  |
|  |  |  |  |  |
|  |  |  |  |  |
|  | |  |  | |
|  |  |  |  |  |

**a.** A. Visu, vitu vinavyongaa, vitu ya kuripuka, kemikali na vyombo vya gesi vilivyokazwa haziruhusiwi.

**b.** B. Vifaa vya mapishi, mikebe ya vyakula, na vibiriti vinaruhusiwa lakini sio lazima, kwani zinaweza kununuliwa baada ya kufika. Wanyama kipenzi wanaruhusiwa, lakini itabidi upange na ulipe garama zozote zinazohusiana na usafiri; kawaida ni rahisi kuacha mnyama kipenzi na jamaa ao katika utunzaji mzuri katika inchi unayotoka.

**c.** C. Viatu, vipodozi, tapi, mavazi na vitabu vinaweza kuwekwa kwa sehemu yako ya mizigo ya kawaida.

**d.** D. Dawa, kompiuta ndogo, vitu vya damani kama vile zahabu na pesa, barua za usafiri, na vyeti ni muhimu na kwa hivyo unapaswa kuzibeba. Nepi, chakula cha watoto, na vitu vingine vidogo vya kibinafsi, kama vile miswaki, unaweza kuzibeba pia.

## Kwa uwanja wa ndege

1. Ubao lililo hapa chini lina majibu ya zoezi.

| a | b | c | d | e |
|---|---|---|---|---|
| v | w | y | z | x |

## Kufika

1. Picha inaelezea ginsi ya kusubiri unapopitia ukaguzi wa pasipoti.
2. Kupitia ukaguzi wa pasipoti inafanyika mbele ya kuchukua mzigo yako
3. Ikiwa barua zako za kibinafsi ziko kwa mizigo yako, hautaweza kuzionyesha kwa eneo la ukaguzi wa pasipoti, kwa hivyo unahitaji kukaa nazo kila wakati.
4. Ili kuhakikisha utambulisho yako vizuri, mamlaka ya Finlande inaweza kukuomba ufungue sikio na shingo yako na pia itachunguza alama za vidole na maelezo yako ya kibinafsi.
5. Ikiwa una pesa ao vitu nyingi ambazo umebeba kwa kusudi la kuziuzisha Finlande, unahitaji kujulisha watu wa Duane. Soma zaidi kuhusu hii kwa site Duane ya Finlande tulli.fi ao usome alama ufuatayo wa QR.

## Kisha ya kufika

1. Majibu yanatofautishana, hata hivi kuwa tayari kuanza kujua luga na kuanza mpango wako wa kujiingiza katika jamii.

# Maisha ya Kila Siku

**Kusimamia maisha ya kila siku**



Je, kuna aina gani ya vyumba katika Finlande? Je, unaweza kununua mboga wapi? Je, unaweza kupata muunganisho wa intaneti vipi? Je, kuna njia gani za usafiri nchini Finlande? Sehemu hii itajibu maulizo haya.

**Katika sehemu hii, utajifunza kuhusu:**

- Nyumba za kupanga
- Facture
- Sheria na kanuni za nyumba
- Takataka na matengenezo
- Maduka na masoko
- Benki
- Usafiri

**Soma kuhusu sehemu hii katika mof.fi/sections/daily_life/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

**Pata sehemu hii mtandaoni katika mof.fi/exercises/daily_life/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

# Nyumba za kupanga

Hebu tusome maandishi na tujibu maulizo.

---

Kama sehemu ya wakimbizi wanaohamia inchi ya tatu, wewe na jamaa yako munastahili nyumba ya kupanga ile itatayarishwa kwa ajili yako katika muji yako.

Ukubwa wa nyumba na hesabu ya vyumba inategemea hesabu ya watu watkaoishi ndani yake, lakini vifaa vya msingi katika nyumba za kupanga kawaida inalingana. Katika nyumba ya kupanga kawaida kuna eneo la mapokezi, mafika, pahali pa kupumzika, vyumba vya kulala, chumba cha kuoga na choo. Katika choo cha Finlande kuna kiti cha choo na sinki ya kunawa mikono. Kawaida kuna chombo kubwa ya kwa kuweka kifukutu ile inaweka nyumba kuwa moto wakati ya baridi. Kila chumba kina kitu ya kuleta kifukutu kinachoweza kubadilishwa.

Mwenye nyumba na mpangaji wanaweka sahihi kwa barua ya upangishaji iliyoandikwa kwa kiwango cha kodi ya upangishaji na muda wa kupanga inaonyeshwa.

---

**1.** Kama sehemu ya wakimbizi wanaohamia inchi ya tatu, ni nani atakayeshurulika kufanya mipango ya kupata nyumba mbele ya kufika kwako kwaFinlande? Ukubwa wa nyumba inategemea nini?

________________________________________

________________________________________

**2.** Je, vifaa vya msingi katika vyumba vinalingana?

________________________________________

________________________________________

**3.** Muji inakusaidia katika kufanya mpango wa kupata nyumba lakini ni nani anayeweka sahihi barua ya upangaji?

________________________________________

**4.** Je, barua ya upangaji ina nini?

________________________________________

________________________________________

**5.** Je, nyumba za kupanga hazina viti, ubao, vitanda?

________________________________________

________________________________________

!

- Nyumba za kupanga inchini Finlande kawaida ina na utumishi za kimsingi tu. Ikiwa unahitaji kitu kamili, lazima ununue wewemwenyewe.
- Utumishi ambazo utapata ukifika kwa nyumba zinaweza kutofautishana. Wenye kusimamia muji wako watakusaidia kuingia kwa nyumba yako mpya ya kupangisha.

# Facture

Hebu tusome maandishi.

---

Kodi ya nyumba inalipwa kila mwezi kwa mwenye nyumba moja kwa moja kupitia kutuma pesa katika akaunti. Kodi isiyolipwa inasababisha kukomeshwa kwa makubaliano ya upangaji.

Mbali na kulipa kodi, kawaida kuna facture tofauti ya maji. Kiasi cha kulipwa kinategemea hesabu ya watu katika nyumba yako. Facture ya maji inakuwa pamoja na matumizi ya kipimo ya maji. Ikiwa utatumia maji kupita kiasi, utapata garama tofauti.

Wapangaji wanapaswa kuweka sahihi kwa barua na mwenye kutoa utumishi za umeme. Facture ya umeme kawaida inalipwa kila mwezi ao mara ine kwa mwaka kupitia kutuma pesa moja kwa moja katika akaunti ya mwenye kutoa utumishi za umeme. Kiasi cha bili ya umeme kinategemea matumizi ya umeme katika nyumba. Ni muhimu kufuatilia matumizi ya maji na umeme, kwa sababu matumizi zaidi yatasababisha garama zaidi.
Wenye kusimamia muji watakusaidia na maswala yanayohusiana na kodi kwa mwanzo.

---

**1.** Jibu kwa "ukweli" ao "uongo".


| | | |
|---|---|---|
| **a** | Kodi inalipwa kupitia kutuma pesa katika benki. | |
| **b** | Ikiwa kodi haijalipwa, ukubaliano wa upangaji utaisha. | |
| **c** | Malipo ya maji kawaida inahesabiwa kando na malipo ya upangaji. | |
| **d** | Malipo ya maji ni sawa bila kujali ni watu wangapi wanaishi katika nyumba. | |
| **e** | Ikiwa maji yanatumiwa kupita kiasi, malipo zaidi yatapaswa kulipwa. | |
| **f** | Facture ya umeme inalipwa kupitia kutuma pesa katika benki. | |
| **g** | Tofauti na malipo ya maji, kiwango cha facture ya umeme hakitegemei hesabu ya watu, lakini matumizi. | |

**2.** Ukurasa ufuatayo una mfano ya facture ya umeme. Hebu tuuangalie pamoja:

- **Sehemu ya 1** ina maelezo yanayohitajika kwa malipo: “eräpäivä” inamaanisha tarehe ambayo malipo yanafaa kulipwa "laskun viite" ni namba ya kukumbuka ile unahitaji kuongeza wakati unalipa ili malipo yako yafuatiliwe.
- **Sehemu ya 2** ina jina lako na adresse yako; kwa njia hii unaweza kuhakikisha kila wakati kuwa facture inatumwa kwako. Siku hizi acture nyingi pia zinatumwa kupitia internet.
- **Sehemu ya 3** ina maelezo kuhusu ukubaliano yako, kwa mfano muda wa ukubaliano yako na ikiwa unapokea facture kila mwezi ao baada ya kila miezi mitatu.
- **Sehemu ya 4** inafupisha maelezo mengi ambayo umesoma hapa juu. Acha tuiangalie na kupata maelezo yanayohitajika.

**!**

- Kulipa kodi na facture kwa wakati ni madaraka yako. Ikiwa hautalipa kwa wakati, utabeba matokeo.
- Unapolipa facture yoyote, unahitaji namba ya akaunti ya benki, jumla ya malipo, na namba ya kukumbuka.
- Ikiwa una maulizo yoyote, usishite kuzungumuza na mamlaka ya kushurulikia.



HELEN

Etunimi Sukunimi
Katuosoite 1 A 11
00100 HELSINKI

Helsingin Energia on nyt Helen Oy

**SÄHKÖLASKU**
12.01.2015 1/4

1. LASKUN TIEDOT
Laskun numero: 12345678
Eräpäivä: 26.01.2015
Laskun viite: 203 12345 12345 12345

2. ASIAKKAAN TIEDOT
Asiakkaan nimi: Etunimi Sukunimi
Asiakasnumero: 1234567
Käyttöpaikan osoite: Katuosoite 1 A 12, 00100 HELSINKI
Käyttöpaikkatunnus: 12345678
Plussakortin numero: 123456 456789 123
Mittarinumero: 12345678

3. SOPIMUKSEN TIEDOT
Sopimusnumero: 123456789
Laskutustapa: 12 kertaa vuodessa
Sopimus voimassa: 26.08.2016 asti
Sähkötuote: Yleissähkö

4.

| | |
|---|---|
| KULUTUSLASKUN YHTEENVETO | |
| KULUTUSLASKU 01.10.2014-31.12.2014 TOTEUTUNUT KÄYTTÖ | 376 kWh |
| Sähköenergia, Yleissähkö Helen Oy | 28,29 e |
| Sähkön siirto, Yleissiirto Helen Sähköverkko Oy | 35,56 e |
| KULUTUSLASKU YHTEENSÄ (SIS. VEROT) | 63,85 e |

5.

| | |
|---|---|
| LASKUN LOPPUSUMMA | 63,85 e |
| Lasku sisältää arvonlisäveroa 51,48 eurosta 24 % | 12,37 e |
| Loppusumma ilman alv | 51,48 e |
| Sähkövero 1.1.2015 alkaen (c/kWh): | |

EDUT Plussaan oikeuttavat ostot 28,29 e.

LASKU | LASKUERITTELY | ASIAKASPALVELU | AJANKOHTAISTA

Saajan tilinumero
IBAN DANSKE BANK FI18 8000 1200 3133 60
POHJOLA FI17 5000 0110 0000 55
BIC DABAFIHH OKOYFIHH

Saaja HELEN Oy
Sähkölasku
Laskun numero: 62680082

Maksajan nimi ja osoite
Etunimi Sukunimi
Katuosoite 1 A 11
00100 HELSINKI

Pyydämme käyttämään maksaessanne tämän laskun viitenumeroa.

Allekirjoitus
Viitenumero 203 12345 12345 12345
Eräpäivä 26.01.2015 Euro 63,85

helen.fi/asiakaspalvelu/kodit/laskutus/laskun-lukuohje/

**a**. Pata na uweke alama ya mviringo kwa tarehe ile inafaa kulipa.

**b**. Pata na uweke alama ya mviringo kwa jumla ya malipo.

**c**. Pata na uweke alama ya mviringokwa kwenye namba ya kukumbuka iliyo ya lazima kuongeza wakati wa kulipa

**d**. Neno "tilinumero" linamaanisha namba ya akaunti. Uipate na uiwekee alama ya mviringo.

# Sheria na kanuni za kawaida

Hebu tusome maandishi na tujibu maulizo.

Kawaida mkimbizi anayehamia inchi ya tatu pamoja na jamaa yake anapanga nyumba katika nyumba la gorofa lenye nyumba nyingi ambazo ni mali ya kampuni ya nyumba. Kila mpangaji wa kampuni ya nyumba anapaswa kutii sheria na kanuni za kampuni yake ya nyumba. Ili utumie chumba cha kufulia ndani ya nyumba, lazima uweke nafasi mapema. Gari inaweza kuwekwa tu pahali iliyotarishwa. Pia, wapangaji wanapaswa kufuata usafi wa nyumba na mazingira na kupanga takataka. Ikiwa kuna kuvunja sheria na kanuni, majirani watalalamikia msimamizi wa kampuni ya nyumba.

**1.** Kampuni ya nyumba ni nini?

**2.** Je, sheria za kampuni zote za nyumba zinafanana?

**3.** Je, unaweza kutumia chumba cha kufulia wakati wowote wakati wa mchana?

**4.** Nani anapanga takataka?

**5.** Je, unaweza kulalamika kwa nani ikiwa kuna mtu alivunja sheria na kanuni?
Je, majirani watalalamika kwa nani ikiwa utavunja sheria?

!

- Nyumba yako ya kupanga ni sehemu ya jengo la gorofa.
- Unahitaji kuheshimu sheria za jengo la gorofa.

# Matengenezo na takataka

Kila kampuni ya nyumba ina utumishi yake ya matengenezo, ambayo unahitaji kuzungumuza naye ikiwa kwa mfano mifereji, shimo la takataka ao vifaa vya kuleta kifukutu vinahitaji kutengenezwa. Ukivumba majia inavia katika nyumba, lazima upigie utumishi ya matengenezo mara moja. Uharibfu yoyote unaotokea ndani nyumba za kupaswa unapaswa kuripotiwa kwa mwenye nyumba. Mwenye nyumba ana mapaswa kurekebisha ao kubadilisha vifaa vilivyoharibika kama vile frigo, fasi ya kupikia ao mifereji. Ikiwa uharibifu umesababishwa na mpangaji, ni yeye atakuwa na mapswa ya kulipia.

**1.** Unganisha sehemu ya swali na sehemu inayolingana ya jibu. Kumbuka kuwa swali linaweza kuwa na majibu mengi na jibu linaweza kuwa sawa kwa maulizo mengi.

| | |
|---|---|
| **a** | ikiwa kitu ya kuleta kifukutu kimevunjika |
| **b** | ikiwa frigo imevunjika |
| **c** | ikiwa nina nia ya kufanya matengenezo yoyote |
| **d** | ikiwa internet haifanyi kazi |
| **e** | ikiwa mifereji ya maji machafu imefungana |
| **f** | kitu ya kutambua moto |
| **g** | ikiwa nina nia ya kubadilisha ukuta ao muundo |
| **h** | ikiwa maji inavia |
| **i** | ikiwa mtu mwingine anahamia kuishi na mimi |
| **j** | ikiwa taa inahitaji kubadilishwa |
| **k** | ikiwa nina swali kuhusu kulipa kodi |
| **l** | ikiwa kitu kimeibiwa |
| **m** | ikiwa ninahitaji vitu za jikoni |
| **n** | ikiwa nilitupa vitu kwa choo na ikafungana |
| **o** | ikiwa nina nia ya kupata mnyama kipenzi |

| | |
|---|---|
| Ninajulisha kampuni ya matengenezo. | **v** |
| ni mapaswa yangu mwenyewe. | **w** |
| Ninajulisha mwenye nyumba. | **x** |
| inapaswa kuwekwa kila wakati kwenye gorofa. | **y** |
| Ninawajulisha Polisi. | **z** |

Mbali na kuchunga nyumba yako katika hali nzuri, una mapashwa ya kuweka mazingira yako ya kuishi kuwa safi. Hebu tusome maandishi na tujue ni ginsi gani unaweza kufanya hivyo.

Kuchunganyumba usafi katika eneo la kampuni ya makazi ni mapashwa ya kila mpangaji. Mifuko yote ya takataka na takataka zinapaswa kupelekwa katika eneo la utupaji taka lililowakwa kwa hili. Kuna maeneo ya utupaji wa takataka kwa uwanja wa kila jengo la gorofa, na wapangaji wanapeleka takataka zao pale. Kampuni nyingi za upangaji zina maeneo tofauti ya utupaji takataka kwa aina tofauti za takataka. Mpangaji anapaswa kupanga takataka na kuweka aina inayofaa katika eneo inayofaa la utupaji wa takataka.



2. Kwa nini tunatumia vitu tena?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

3. Kwenye ubao lifuatalo, unaweza kuona aina tofauti za takataka na picha ya mfano ya kila aina ya takataka. Weka vitu ifuatavyo kwa pipa inayofaa. Soma sanduku kwa mwisho wa ukurasa.

Mavi ya wanyama kipenzi | Mimea iliyokauka | Gazeti | Nepi | Vyombo vya chupa | Mikebe ya plastike | Chuma kilichovunjika | Katoni za ufungaji | Mikebe ya mbaazi | Chombo cha karto | Taulo za usafi | Magazeti | Mabaki ya vyakula | Maganda ya ndizi | Chupa | Mikebe ya nyanya | Chupa za plastiki zisizowekewa garati | Mavazi yaliyoraruka | Plastiki za ufungaji | Maganda ya karoti | Takataka zingine ambazo sio sehemu ya aina yoyote

| | | |
|---|---|---|
| Takataka hatari kwa mazingira |  | |
| Karatasi |  | |
| Karto |  | |
| Chuma |  | |
| Chupa |  | |
| Plastiki |  | |
| Takataka iliyochanganywa |  | |

4. Tembelea kierratys.info ili upate maelezo zaidi kuhusu ginsi ya kutumia tena vitu.

!

- Chupa za plastiki na glasi ambazo zinawekewa garati zinaweza kurudishwa sokoni na unaweza kurudishiwa pesa za garati.
- Vitabu vya zamani vinaweza kutolewa kwa fasi ya kusoma vitabu na mavazi ya zamani yanaweza kutolewa kwa vituo vya ukusanyaji.
- Betri, taa fulani, kompiuta, simu, vifaa vya zamani vya elektroniki, rangi, na vitu vingine vyenye hatari haviwezi kutupwa na lazima virudishwe kwenye vituo vya ukusanyaji.
- Utumiaji tena ya vitu unafanya inchi iwe safi; ni mapashwa yako kama mkaajii wa muji na raia wa baadaye kuweka Finlande iwe safi.

# Kununua katika muji yako

Maandishi yafuatayo yametolewa kutoka kwa ukurasa ya site ya somo. Kiungo cha ukurasa huu inaweza kupatikana kwa mwanzo ya sehemu hii. Umeiipata? Inakaa hivi mof.fi/sections/daily_life/en na unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu jambo kutoka hapa.
Hebu tusome maandishi.

---

Watu inchini Finlande wananunua vyakula na vitu vingine vya vyakula kawaida kutoka kwa maduka makubwa na maduka makuu. Katika maduka makuu pia kuna maduka ya mavazi na viatu. Unapoingia kwa duka unachukua troli ya ununuzi ao kikapo cha ununuzi ili kukusanya ununuzi wako ndani yake. Maduka hayo yana sehemu tofauti za vitu tofauti. Katika sehemu ya mboga na matunda unaweza kukusanya kiasi cha matunda na mboga unazotaka kwenye karatasi ao mifuko ya plastiki. Kisha ya kukusanya, weka mufuko ya matunda ao mboga ya mashine ya kilo, kisha finya namba ya vitu na mashine inakupa bei. Unaweka alama ya bei kando ya mufuko. Unaweza kununua mkate kwa sehemu ya mikate. Samaki na nyama kawaida zinaulizwa kwa kaunta kwa ajili ya vitu hizi. Mavazi na viatu vinaweza kupatikana dukani na alama za bei zinawekwa kwa vitu. Malipo inafanywa kwa kaunta na pesa ao kwa kadi ya benki.

Katika miji ndogo na kubwa unaweza kupata maduka ya kuuza vitu zinazotumiwa zaidi na wahamiaji. Miji ndogo na kubwa zina soko wapi unaweza kununua matunda, mboga, beri na samaki kati ya vitu zingine, na kutumia wakati na watu wa karibu na kunywa kahawa.

Masoko yanayofanyika inje yana mavazi mengi kwa watoto na watu wazima, vifaa vya nyumba, ubao, viti, vitanda, na vifaa ya michezo kwa watoto zile ziko katika hali nzuri. Mavazi zile hazijatumiwa sana kwa watoto wadogo pia zinapatikana sana. Pata kujua soko zako za karibu zinazofanyika inje mbele ya kununua vitu mpya. Kwa kununua vitu zilizotumiwa unaweza kuokoa pesa mingi kwa matumizi ya nyumba yako.

Kwa Finlande karibu kila mtu, iwe watoto, vijana, watu wazima na wazee, wanatumia simu za mkono. Unaweza kununua kadi ya SIM unayolipia mbele ya kutumia utumishi kutoka kwa R-kioski ya eneo lako ao unaweza kupata SIM kadi kutoka kwa kampuni ya simu na ulipe facture kila mwezi.

---

**1.** Jibu kwa "Ukweli" ao "Uongo".

| | | |
|---|---|---|
| **a** | Matunda na vitu za usafishaji zinapatikana katika sehemu tofauti za duka. | |
| **b** | Malipo yanaweza kufanywa ukitumia kadi ya benki. | |
| **c** | Inchini Finlande kuna maduka zile zinauzisha vitu za kigeni na vitu zinazotumiwa zaidi na wahamiaji. | |
| **d** | Vitu kutoka soko zinazofanyika inje ni kali zaidi kuliko zile katika maduka mengine. | |
| **e** | Kwa kununua kutoka kwa soko zinazofanyika inje unaweza kuokoa pesa mingi ya nyumba. | |
| **f** | Maduka ya R-kioski zinauzisha kadi za SIM unazolipia mbele ya kutumia utumishi. | |

**2.** Soko mengi zinazofanyika inje zinaweza kupatikana mtandaoni. Jaribu kutafuta sites zile zina neno "kirpputori". Unaweza pia kutafuta vikundi na kurasa kwenye mitandao ya kijamii ambazo zinaweka neno "kirpputori". Shiriki matokeo na marafiki wako ao jamaa.

**!**

- Kwa kawaida hakuna mabishano ya bei katika maduka inchini Finlande, isipokuwa katika soko zinazofanyika inje.
- Katika fasi ya kutumia tena itu, unaweza kupata vitu bora kwa bei muzuri.
- Unaweza kufikia internet kupitia kujiandikisha na SIM unayolipia mbele ya kutumia utumishi, kati ya zingine. Uliza kuhusu chaguo tofauti za inernet na ginsi ya kuzipata.

# Benki

Kuchunga pesa yako vizuri ni jambo muhimu katika maisha yako ya kila siku inchini Finlande. Katika sehemu hii, utajifunza kuhusu ginsi ya kutumia utumishi za benki inchini Finlande. Hebu tusome maandishi.

Ni muhimu kwa kila mhamiaji mtu mzima kufungua akaunti yake ya benki katika muji wake ao katika muji ya karibu. Pasipoti halali, ukubali ya kuishi, na kujiandikisha kwa muji zinahitajika kwa hii. Mara tu kisha akaunti kufunguliwa utapata kadi ya kibinafsi ya benki. Ukiwa na kadi yako ya benki unaweza kutoa pesa kutoka kwa mashine za pesa na kulipia vitu umenunua kwa maduka. Hakikisha unakumbuka namba ya siri (PIN) ya kadi yako ya benki. Namba ya PIN ni namba ya hesabu ine ile utapata kutoka benki.

Unaweza kutoa pesa kutoka kwa mashine za pesa katika yuro, iliyo sarafu ya Finlande na katika inchi zingine nyingi za Ulaya. Inchini Finlande, njia ya malipo ya kawaida ni kadi ya benki. Unaweka kadi yako ya benki kwa mashine ndogo dukani kisha unaweka namba ya PIN yako. Garama ya ununuzi yako itatolewa kiotomatiki kutoka kwa akaunti yako. Unaweza pia kulipa na pesa.

**1.** Akaunti ya benki ni nini?

**2.** Unaweza kutumia akaunti yako ya benki namna gani?

**3.** Kadi ya benki ni nini?

**4.** Unaweza kutumia akaunti yako ya benki namna gani?

Pamoja na kadi ya benki, benki itakutumia vitambulisho vya benki au kukupa njia ya kuzipata. Vitambulisho vyako vya benki ni namba inayotumiwa kufanya malipo ya mtandao ao kupata utumishi zingine za mtandao na wakati mwingine kufanya utambulisho wako kwenye site fulani. Vitambulisho vya benki huitwa "pankkitunnukset" katika Kifini.

**5.** Unaweza kufanya nini na vitambulisho vyako vya benki?

**6.** Unapata wapi vitambulisho vya benki?

!

- Kila mtu, wanaume, wanawake na watoto wana akaunti zao. Malipo inafanywa kwa akaunti ya mtu huyo.
- Daima weka kadi yako ya benki na vitambulisho vya benki nafasi salama.
- Namba ya PIN ya kadi yako ya benki ni ya kibinafsi. Usiionyeshe kwa wengine.

# Usafiri

Usafiri ni sehemu muhimu ya maisha. Hebu tujifahamishe njia za usafiri nchini Finlande kwa kusoma maandishi na kujibu maulizo.

Njia za usafiri ya watu wengi (uma) katika eneo ni pamoja na mabasi za eneo, treni za eneo na tramu. Njia za usafiri ya uma kwa safari za mbali mabasi na treni za safari marefu. Kutumia usafiri wa uma kawaida ni bei muzuri ikilinganishwa na kutumia gari la kibinafsi.

**1.** Je, ina malipo kidogo kusafiri kwa kutumia usafiri wa uma?

**2.** Je, kuna njia zingine za usafiri wa uma katika inchi yako tofauti na zile za Finlande?

Watu wanangoja mabasi ya eneo kwa vituo vya mabasi ambavyo vimewekwa alama za kusimama kwa basi, na ambapo mabasi yanasimama kuchukua wasafiri. Wakati basi inafika kwenye kituo cha basi, lazima utoe alama kwa dereva wa basi ili aweze kusimama. Katika miji mingi pesa inalipwa kwa kutumia kadi ya basi ile abiria anaweka pesa ndani yake mbele. Ikiwa hauna kadi ya basi unaweza kulipa na pesa kwa mkono. Mabasi ya safari marefu zinachukua asafiri kutoka vituo vya mabasi vilivyowekwa kwa mabasi ya safari marefu. Bei ya safari marefu kawaida ni muzuri ikiwa utanunua tikiti mapema mtandaoni.

**3.** Usafiri katika eneo ni salama. Watoto wanaweza kuutumia kwenda shuleni, na wakati mwingine wanapata punguzo la bei. Je, hili lipo katika nchi yako?

**4.** Katika miji mengi, lazima utumie kadi ya usafiri ambayo tayari imewekwa pesa. Ikiwa hauna kadi, unaweza kulipa namna gani?

**5.** Unaposafiri kwa safari marefu, bei ya kununua tikiti mapema kawaida ni muzurikwa kuliko kununua kwenye basi. Wakati ingine njia pekee ya kununua tikiti ni mbele ya safari. Je, ni vivyo hivyo katika inchi yako?

**6.** Ukurasa unaofuata una ramani tatu. Ni ramani gani inaonyesha barabara kuu inchini Finlande? Zungumuza na jamaa yako ao wenzako. Ramani imetolewa kwa wikipedia.com.

**!**

- Usafiri ni salama kwa wanawake, watoto na wanaume.
- Kununua tikiti kutoka kwa internet ao mapema kwa kawaida ni bei muzuri.
- Wahamiaji mara mingi wanahitaji kuwa na ruhusa ya udereva ya Finlande kabla ya kuruhusiwa kuendesha gari inchini Finlande. Tembelea traficom.fi ili upate maelezo zaidi kuhusu ruhusa ya udereva.

Treni zinasafiri maeneo mengi kote Finlande. Miji ndogo zote na mikubwa zina vituo vya treni. Treni zinasimama kwa vituo vya treni wapi abiria wanaweza kuondoka na kuingia kwa treni. Kwa kawaida, tikiti inanunuliwa kutoka kituo cha treni, lakini pia inaweza kununuliwa kutoka kwa internet na wakati ingine ndani ya treni.

**7.** Unaweza kununua tikiti za treni wapi?


**8.** Hapo chini kuna ramani tatu. Ni ramani gani ndio inayoonyesha reli inchini Finlande? Zungumuza na jamaa yako ao wenzako. Chanzo cha ramani ni www.vr.fi; tafazali tembelea site.

**9.** Ramani iliyobaki inaonyesha nini? Ramani imetolewa kwa wikipedia.com.

Katika Finlande watu wanaendesha baiskeli sana. Watu wengi wanaendesha baiskeli kwenda darasani na kazini. Baiskeli zinawekwa katika maeneo ya kuweka baiskeli. Wakati wa kuendesha baiskeli, ni muhimu kufuata sheria za barabara na kutumia kofia ya kuchunga kichwa. Mtu anayeendesha baiskeli lazima wajali wale wanaotembea na kuvuka barabara.

**10.** Watu huendesha baiskeli sana inchini Finlande; ni salama na kawaida kwa wanawake na wanaume na watoto pia. Je, ni kawaida katika inchi yako? Je, unafikili utaendesha baisikeli inchini Finlande?

**11**. Je, ni mambo gani matatu unazohitaji kukumbuka unapoendesha baiskeli?









# Uvutaji sigara

Hebu tusome maandishi.

Uvutaji sigara katika maeneo yote ya uma; katika viwanja vya ndege, vituo vya treni, vituo vya mabasi, shule, ofisi, na kwa mabasi, treni, ndege na barabara za chumba kubwa umekatazwa na sheria. Kuna maeneo tofauti, yaliyowekwa alama wazi zile zimewekwa kwa uvutaji sigara katika maeneo ya uma. Lazima utumie maeneo haya wakati ya kipwa na ya baridi pia. Sehemu zinazobaki za sigara zinapaswa kuwekwa kwa pipa la takataka hio.

**1.** Kwa maoni yako, ni sehemu gani kati ya hizi unaweza kuvuta sigara na wapi hauwezi? Angalia majibu ili kujua ni sheria gani katika Finlande.

| | | |
|---|---|---|
| Kwa basi | | |
| Katika ua | | |
| Nyumba yako mwenyewe | | |
| Gari yako ukiwa na watoto | | |
| Bustani | | |
| Nafasi iliyowekwa alama kama eneo lisilo la uvutaji sigara | | |
| Nafasi iliyowekwa alama kama eneo la uvutaji sigara | | |
| Ndegeni | | |
| Mtaani | | |

Kwa kuwa umemaliza sehemu, andika mawazo kama atano kuhusu mambo mapya ambayo umejifunza. Mawazo hayapaswi kufanana na yale yaliyo kwa sanduku linalopatikana hapa chini lakini unaweza kuyatumia ili kupata wazo jipya. Gawa maoni yako na jamaa yako au marafiki.

- Kama mkimbizi anayehamia inchi ya tatu, utaishi katika nyumba ya ukodishaji.
- Ni madaraka yako kulipa kodi na facture kwa wakati.
- Ni jukumu lako kuchunga nyumba hii katika hali nzuri na kuweka mazingira yako iwe safi.
- Karibu malipo yote zinafanywa kupitia benki yako ya internet na kadi yako ya benki. Malipo ya pesa kwa mkono si ya kawaida.
- Kuna chaguo nyingi kwa kununua.
- Mtandao wa usafiri wa uma ni mzuri sana.
- Uvutaji sigara katika maeneo yote ya uma inakatazwa.

# Majibu

## Kupanga

1. Katika Finlande utaishi katika nyumba ya kupanga ile mujiw yakoako imekutayarishia. Ukubwa wa nyumba unategemea hesabu ya watu wanaoishi ndani.
2. Vifaa vya msingi katika kila nyumba vinafana.
3. Wewe, kama mpangaji, utaweka sahihi kwa barua ya makubaliano ya kupanga na mwenye nyumba.
4. Barua ya makubaliano ya kupanga ina bei ya kulpa kwa kupanga na urefu wake ya upangaji.
5. Nyumba za kupanga hazina viti, ubao, vitanda.

## Facture

1. Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| a | b | c | d | e | f | g |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukweli | Ukweli | Ukweli | Uongo | Ukweli | Ukweli | Ukweli |

2. Majibu yanaweza kupatikana kwenye picha.




## Sheria na kanuni za kawaida

1. Kampuni ya nyumba inamiliki jengo la gorofa wapi nyumba yako iko.
2. Kila kampuni ya nyumba ina sheria zake. Kila mpangaji wa kampuni ya nyumba anapaswa kutii sheria na kanuni za kampuni yake ya nyumba.
3. Chumba cha kufulia katika kampuni ya nyumba kinaweza kutumika tu kwa nyakati zilizowekewa nafasi.
4. Wapangaji wanapaswa kuweka usafi wa jumla wa mazingira na upangaji wa takataka.
5. Ikiwa kuna malalamiko ao kuvunja sheria, unapaswa kuzungumuza na kampuni ya nyumba.

## Matengenezo na takataka

1. Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

<table>
<tr><th>a</th><th>b</th><th>c</th><th>d</th><th>e</th><th>f</th><th>g</th><th>h</th><th>i</th><th>j</th><th>k</th><th>l</th><th>m</th><th>n</th><th>o</th></tr>
<tr><td>v | x</td><td>x</td><td>x</td><td>w</td><td>v</td><td>y</td><td>x</td><td>v | x</td><td>x</td><td>w</td><td>x</td><td>z</td><td>w</td><td>w</td><td>x</td></tr>
</table>

2. Utumiaji tena ya vitu ni muhimu ili kulinda mazingira yako na kuyaweka safi. Utumiaji tena ya vitu unamaanisha kubadilisha kitu kuwa tena ya mwanzo ili inaweza kutumika tena.

**3.** Majibu yanaweza kupatikana kwenye ubao ufuatayo.

| | |
|---|---|
| Takataka hatari kwa mazingira | Mimea iliyokauka \| Mabaki ya chakula \| Maganda ya ndizi \| Maganda ya karoti |
| Karatasi | Magazeti \| Magazeti |
| Karto | Karto za ufungaji \| Chombo cha karto cha juu ya nyumba |
| Chuma | Mkebe wa jodari \| Chuma kilichovunjika \| Mkebe wa mbaazi \| Mkebe wa nyanya |
| Chupa | Vyombo vya chupa \| Chupa za glasi |
| Plastiki | Chupa za plastiki zisizowekewa pesa ya garati \| Plastiki za ufungaji |
| Takataka iliyochanganywa | Mavi ya wanyama kipenzi \| Nepi \| Taulo za usafi \| Mavazi yaliyoraruka \| Takataka zingine zozote zile haziko katika aina hizi |

**4.** Site ya kierratys.info ina maelezo muhimu kuhusu vituo vya kutumia tena vitu na ukusanyaji. Tembelea na ujue wale walio karibu nawe.

## Kununua katika muji yako

**1.** Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| a | b | c | d | e | f |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukweli | Ukweli | Ukweli | Uongo | Ukweli | Ukweli |

**2.** Majibu yanatofautishana.

## Benki

**1.** Akaunti ya benki ni akaunti ile unapata kutoka kwa benki. Akaunti ya benki ina namba ya akaunti.
**2.** Akaunti ya benki inaweza kutumika kuhamisha na kupokea pesa.
**3.** Kadi ya benki ni kadi ya plastiki ile unapata kutoka kwa benki. Inaweza kugarimu pesa kupata kadi ya benki. Picha ifuatayo ni mfano wa kadi ya benki.




**4.** Ukiwa na kadi yako ya benki unaweza kutoa pesa kutoka kwa mashine ya pesa na kulipia vitu umenunua kwa maduka.
**5.** Vitambulisho vya benki vinaweza kutumiwa kufanya malipo ya mtandao ao kupata utumishi zingine za mtandao zinazohusiana na benki na wakati mwingine kufanya utambulisho yako kwa ite fulani.
**6.** Benki itakutumia vitambulisho vyako vya benki. Vitambulisho vya benki pia vinaweza kutumiwa kupitia simu yako. Picha iliyo kwa kuume ni mfano ya vitambulisho ya benki.



## Usafiri

1. Kusafiri kwa njia ya usafiri ya uma kwa kawaida ina bei muzuri.
2. Majibu yanatofautishana.
3. Majibu yanatofautishana.
4. Ikiwa hauna kadi ya usafiri ya basi unaweza kulipa na pesa kwa mkono. Siku hizi unaweza pia kulipa kwa simu yako katika miji zingine.
5. Majibu yanatofautishana.
6. Ramani ya "a" inaonyesha barabara kuu inchini Finlande. Barabara zenye rangi nyekundu ni barabara za kiwango cha kwanza ao "valtatiet" na zile zenye manjano ni za kiwango cha pili ao "kantatiet"
7. Tikiti inaweza kununuliwa kutoka kituo cha treni, ao kutoka kwa internet. Katika treni nyingi, tiketi zinaweza pia kununuliwa ndani ya treni. Watu wengi siku hizi wananunua tikiti ya treni kwa internet. Pia kuna programe za simu za mkono zinazopatikana ili kununua tikiti kwa internet. Angalia ginsi utumishi hii unavyofanya kazi katika muji wako!
8. Ramani ya "c" inaonyesha reli inchini Finlande. Unaweza kununua tikiti za treni katika site ya vr.fi.
9. Ramani ya "b" inaonyesha viwanja vya ndege inchini Finlande.
10. Majibu yanatofautishana.
11. Wakati wa kuendesha baiskeli, ni muhimu kufuata sheria za barabara, kutumia kofia ya kuchunga kichwa, na kujali wale wanaotembea na kuvuka barabara.

## Uvutaji sigara

1. Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| Kwa basi | Katika ua | Nyumba yako mwenyewe | Gari ukiwa na watoto | Bustani |
|---|---|---|---|---|
|  |  |  |  |  |

| Nafasi iliyowekwa alama kama eneo lisilo la uvutaji sigara | Nafasi iliyowekwa alama kama eneo la uvutaji sigara | Ndegeni | Mtaani |
|---|---|---|---|
|  |  |  |  |

# Masomo

**Shule na Masomo**



Ninaweza kumaliza masomo yangu wapi? Watoto wangu wanaweza kusomea wapi? Je, nitaanza kusoma mara tu kisha ya kufika Finlande? Haya yote ni katika sura hii.

**Katika sehemu hii, utajifunza kuhusu:**

- Utumishi ya utunzaji wa watoto ya mcha na masomo ya mbele
- Shule ya jumla
- Shule za sekondari
- Masomo ya ufundi na majifunzo
- Masomo ya Juu
- Majifunzo ya kujiingiza katika jamii kwa wahamiaji
- Majifunzo ya soko ya kazi kwa watu waz
- Kulinganisha diplomes
- Pahali pa kusoma vitabu

**Soma kuhusu sehemu hii katika mof.fi/sections/education/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

**Pata sehemu hii mtandaoni katika mof.fi/exercises/education/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

# Utumishi ya utunzaji wa watoto ya mchana na masomo ya mbele

Kama wakaaji wa muji, unaweza kutuma maombi kwa ajili ya nafasi ya utunzaji wa watoto wako. Katika vituo vya utunzaji ya mchana, watoto watajifunza luga ya Kifinlande, mambo ya kila siku na kujua umuhimu wa kijamii. Ratiba ya kila siku ya vituo inakuwa vile na shuruli za ndani na inje kama vile michezo, mazoezi, muziki, sanaa na ufundi, na muda wa kula pamoja. Malipo ya utunzaji ya mchana inategemea mapato ya jamaa. Watoto mara mingi wanacheza inje, na lazima wazazi waende kuwachukua kwa hivi wazazi wanapaswa kujitayarisha kwa kuwavalisha watoto kulingana na hali ya hewa. Watoto wana haki ya kupata masomo ya mbele kwa mwaka moja mbele ya kuanza masomo yao ya lazima ya msingi, kwa jumla wakiwa na umri wa miaka sita. Katika masomo ya mbele, watoto watapata maarifa na kujua ile itasaidia hatua yao ya masomo katika shule ya jumla.

**1.** Soma maandishi na ukamilishe tangamano na jibu sawa.

**a.** Masomo ya mbele inachukua ___________________________.

mwaka moja | miaka mbili | miaka tatu

**b.** Malipo ya utumishi ya utunzaji ya watoto ___________________________________________________.

inalingana kwa kila mtu | inategemea mapato ya jamaa

**c.** Watoto lazima wavalishwe mavazi yanayofaa ______________________________.

shuruli za ndani | shuruli za inje | shuruli za ndani na inje

# Shule ya jumla

Hebu tusome maandishi.

Watoto wote wanaoishi kwa kudumu inchini Finlande wana haki ya kupata masomo ya msingi ya lazima. Haki hii inaanza kwa umri wa miaka 6 kwa masomo ya mbele. Kisha hii, watoto wanaanza shule ya jumla inayodumu kwa miaka 9 na kuwapa watoto masomo ya msingi. Kwa jumla watoto wanaanza shule ya jumla wakiwa na umri wa miaka 7 na kumaliza wakati programe ya lazima inapokamilika, kawaida wakiwa na umri wa miaka 16. Shule ya jumla ina masomo ya mbele, cha msingi na kiwango cha sekondari ya chini. Kiwango cha msingi ni pamoja na darasa kuanzia 1 hadi 6 na kiwango cha sekondari ya chini ni pamoja na darasa kuanzia 7 hadi 9. Wazazi wana mapashwa ya kuhakikisha kuwa watoto wao wanahuzuria shule kila siku.

**1.** Jibu kwa "Ukweli" au "Uongo" na ueleze ni kwa nini.

**a.** Ni watoto wa asili ya Finlande pekee yao wanalazimika kupata masomo ya msingi, kwa watoto wahamiaji ni si ya lazima.

___________________________________________________

**b.** Masomo ya lazima inaanza kwa daraja 1 hadi 6 pekee.

___________________________________________________

**c.** Wazazi wana madaraka kufuatilia watoto wao shuleni.

___________________________________________________

Watoto wanasoma masomo mengi ya lazima katika shule ya jumla, kama vile hesabu, Kufunlande, Kizungu, historia, biolojia, na kazalika. Wanafunzi wote katika shule za Finlande wanashiriki katika masomo ya kimwili na masomo ya sanaa. Kuna sanaa na ufundi mingi shuleni, na vifaa vya kuona vinatumiwa sana katika kufundisha. Kawaida mwanafunzi huagizwa ainue mkono wakati anapoomba ruhusa ya kuzungumza darasani. Luga tofauti zinasomwa shuleni.

Watoto wa Finlande hawana nguo za shule; kwa hivyo wazazi wanapasha kuhakikisha watoto wao wana mavazi yanayofaa na mazuri zile zinafaa kwa wakati na hali ya hewa. Kwa madarasa ya michezo na masomo ya kimwili, watoto lazima wawe na mavazi na viatu vya michezo. Madarasa katika shule za Kifini hudumu kwa muda wa takriban dakika 45. Kuna mapumziko ya dakika 15 kati ya madarasa, na mara moja kwa siku mapumziko marefu ya chakula cha mchana ambapo chakula hutolewa.

**2.** Unganisha sehemu ya kwanza na sehemu inayolingana ya pili.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | Wanafunzi wote wanashiriki | katika madarasa ya michezo na sanaa. | **w** |
| **b** | Wazazi wana mapashwa kwa watoto wao kuwa na mavazi yanayofaa | kwa kuinua mkono wako. | **x** |
| **c** | Kuomba ruhusa ya kuzungumza darasani kunafanywa | kwa hali ya hewa na michezo. | **y** |
| **d** | Madarasa hudumu kwa dakika 45 | na inafuatwa na mapumziko ya dakika 15. | **z** |

Watoto wahamiaji ale wamefika tu Finlande wanapata majifunzo ya mwanzo ile inawatayarisha kwa shule ya jumla. Wanafunzi wanasoma luga ya Kifinlande na masomo mengine, na kuimarisha kujua kwao ya kusoma na kuandika. Katika shule ya jumla, mtoto mhamiaji anawekwa kwa daraja linalofaa zaidi umri, maarifa na kujua kwake. Ao, majifunzo katika masomo mbalimbali yanaweza kupangwa kwa ajili ya wageni. Dini pia ni somo katika shule ya jumla na shule ya sekondari katika Finlande. Mafundisho yake yamepangwa kulingana na uwingi ya dini.

**3.** Wanafunzi wahamiaji wanapata mafundisho ya mambo ya sasa (mode) pia katika Kifinlande. Je, hii inaleta faida gani kwa maoni yako?

4. Mafundisho ya kidini yamepangwa kulingana na dini ya watu wengi, na bado wazazi wa mtoto wana haki ya kuomba mafundisho ya kidini kulingana na dini yao, na yataweza kupangwa **ikiwezekana**. Kuliko mafundisho ya dini, watoto wanaweza pia kushiriki katika mafundisho ya mambo ya sasa (modes). Je, unazani wazazi wanapaswa kuomba mafundisho ya imani yoyote kwa watoto yao? Je, maoni yako ni gani kuhusu mafundisho ya kidini inchini Finlande? Je, unazani yana tofauti fulani ikilinganishwa na ile ulizoea mbele?

______________________________

______________________________

**!**

- Iwe katika masomo ya mbele ao katika shule ya jumla, wazazi wana mapashwa muhimu katika kusaidia masomo ya watoto wao.

5. Kwa ubao ifuatayo, kuna maelezo kuhusu mambo fulani yale ulizoea. Toa maoni yako ikiwa mambo haya yanaweza kupatikana inchini Finlande ao hapana, na maoni yako kuhusu mambo haya na kwa nini

| | | Yanatokea inchini Finlande | Maoni na uhalali |
|---|---|---|---|
| **a** | Wasichana na wanaume wanasoma pamoja | | |
| **b** | Wanafunzi wanatumia jina la kwanza ya mwalimu | | |
| **c** | Kula chakula cha mchana shuleni | | |
| **d** | Azabu | | |
| **e** | Wazazi wanafuatilia masomo ya watoto wao | | |
| **f** | Wanafunzi wanasimama wakati mwalimu anapoingia | | |
| **g** | Kuvaa nguo ya shule | | |
| **h** | Kusoma zaidi ya masaa sita kwa siku | | |
| **i** | Madarasa ya kuogelea | | |

**6.** Kama mwanafunzi, unaweza kukutana na hali zingine zile ni mpya kwako. Hapa kuna mifano fulani zile zinaweza ao zisiyoweza kutokea. Unaweza kufanya nini?

| | | |
|---|---|---|
| **a** | Mtu amenyanyaswa ao kuchokozwa shuleni. | |
| **b** | Mwalimu anataka kukutana nawe. | |
| **c** | Huelewi jambo fulani katika somo | |
| **d** | Kitu kilichotokea nyumbani na umeshindwa kufanya kazi yako ya nyumbani | |
| **e** | Mwanafunzi amekuomba mukule pamoja. | |

**7.** Kama mzazi, utazungumuza kila wakati na waalimu wa watoto wako. Hapa kuna mifano ya hali zinazoweza kutokea ao kukosa kutokea. Unaweza kufanya nini?

| | | |
|---|---|---|
| **a** | Mwalimu anataka kukutana nawe. | |
| **b** | Mtoto wako anahitaji kushiriki katika mambo yale haukubaliane nazo. | |
| **c** | Mtoto wako hajafanya kazi ya nyumbani aliyopewa. | |
| **d** | Mtoto wako ana tabia mbaya shuleni. | |
| **e** | Mtoto wako amefanya maendeleo mazuri shuleni. | |
| **f** | Mtoto wako hataki kwenda shule. | |

# Shule ya sekondari ya juu

Maandishi yafuatayo yametolewa kutoka kwa ukurasa ya site ya somo. Kiungo cha ukurasa huu inaweza kupatikana kwa mwanzo ya sehemu hii. Umeiipata? Inakaa hivi mof.fi/sections/education/en na unaweza kupata maelezo mengi yale yatakusaidia kupata majibu ya zoezi zifuatazo.

---

Mtu anaweza kuomba masomo ya sekondari ya juu kwa kutumia cheti cha kukamilisha shule kutoka kwa shule ya jumla. Masomo yanaweza kukamilika kati ya miaka 2 hadi 4. Lengo la masomo ni mitihani ya mwisho ya kitaifa, wapi yale mwanafunzi alijifunza kwa jumla inachunguzwa kwa kiwango kubwa. Kisha kumaliza shule ya sekondari ya juu mwanafunzi anapokea diplome. Kisha kumaliza mitihani ya kuingia katika chuo kikuu, mwanafunzi pia anapokea cheti cha mtihani wa kuingia chuo kikuu. Masomo ya shule ya sekondari ya juu yanahitajika kwa masomo ya masomo ya juu.

---

**1.** Shule ya sekondari ya juu inafanyika wakati gani?

---

**2.** Shule ya sekondari ya juu inachukua muda gani?

---

**3.** Je, ni kiwango gani cha masomo kinachohitaji ukamilishe masomo ya sekondari ya juu?

---

# Majifunzo ya ufundi

Hapo chini kuna aya mbili kuhusu masomo ya ufundi, hebu tuzisome.

| Masomo ya ufundi na majifunzo | Majifunzo ya ufundi ya matayarisho kwa vijana wahamiaji |
|---|---|
| Hesabu kubwa ya nafasi ya majifunzo za ufundi inchini Finlande zinatoa chaguo nyingi za mipango ya masomo ya ufundi na majifunzo, zile zinatoa kujua kwa kazi za vitendo. Katika masomo ya ufundi, kijana anaweza kusoma na kupata kujua ufundi, ile inachukua karibu miaka 2 hadi 3. Masomo ya ufundi inakuwa pamoja na vitendo sana. Wanafunzi anafuata vipindi vya wanafunzi na masomo ya vitendo katika sehemu tofauti za kazi. Mtu anaweza kuomba majifunzo ya ufundi, kwa kutumia cheti cha kukamilisha shule kutoka kwa shule ya jumla ao na cheti sawa cha masomo. Kwa sababu luga ya mafundisho katika mipango ya majifunzo ya ufundi ni Kifinlande, ni muhimu kujifunza Kifinlande katika kwa mwanzo ikiwezekana. | Kisha ya kukamilisha masomo ya jumla, mtu anaweza kuchagua ao shule ya ufundi ao shule ya sekondari ya juu. Ikiwa kijana mhamiaji anahitaji masomo zaidi ya luga ya Kifinlande ao Kiswidi ao masomo mengine ya msingi, anaweza kufuata daraja la 10 katika masomo ya jumla ao mwaka moja katika majifunzo ya ufundi ya kujitayarisha. Katika majifunzo ya ufundi ya matayarisho mwanafunzi anaimarisha kujua kwake ya luga. Mwanafunzi pia anasoma hatua za maisha na kazi tofauti, na anajitayarisha kwa masomo zaidi ya ufundi. Wakati wa majifunzo ya kujitayarisha mwanafunzi atakuwa na bahati ya kutambua nguvu na mapendeleo yake ya ufundi. |

1. Shule ya ufundi inafanyika wakati gani?

2. Kuna tofauti gani kati ya masomo ya ufundi na sekondari ya juu?

3. Majifunzo ya ufundi ya matayarisho kwa vijana wahamiaji ni nini?

4. Hapa chini utapata oroda ya sifa. Tambua nini ni mambo kamili kwa majifunzo ya ufundi ya kutayarisha vijana wahamiaji na ni nini ni ya kawaida?
   **a.** Inatayarishe kwa ufundi
   **b.** Inaleta nguvu kujua luga ya Kifinlande
   **c.** Unaweza kuingia kwa kutumia cheti cha kukamilisha shule ya jumla ao cheti sawa
   **d.** Inatayarisha kwa masomo ya ufundi

5. Kisha ya masomo ya ufundi, unaweza kuanza kufanya kazi mara moja ao unahitaji masomo zaidi?

# Masomo ya juu na vyuo vikuu

Hebu tusome sehemu hii ndogo kutoka kwa ukurasa wa somo.

> Katika Finlande, masomo ya juu inaweza kupatikana katika vyuo vikuu vya sayansi tu. Masomo yanaweza kukamilika kati ya miaka 3 hadi 4 ao 5. Masharti ya kujiandikisha ni cheti cha sekondari ya juu ao cheti cha masomo ya ufundi. Diplome mingi za chuo kikuu ni pamoja na diplome ya kwanza, ikifuatiwa na ya pili. Kunaweza kuwa na mitihani ya kustahili kuingia kwa programe za masomo ya juu.


1. Ukweli ao uwongo?
   **a.** Unaweza kujiunga na masomo ya juu tu kutoka shule ya sekondari ya juu.

   **b.** Masomo ya juu inapatikana tu katika vyuo vikuu vya sayansi.

   **c.** Diplome mingi za chuo kikuu ni pamoja na diplome ya kwanza na ya pili.

- Baada ya shule ya jumla, mtu anaweza kuchagua kujiunga na sekondari ya juu ao shule ya ufundi. Kila moja ina faida yake.
- Shule ya ufundi ni kwa wale wanataka kuanza maisha ya kifundi. Shule ya sekondari ya juu ni kwa wale wanataka kusoma zaidi. Umepewa chaguo.
- Ikiwa unahitaji usaidizi kwa luga yako na kujua ingine, unaweza kupata mwaka zaidi ya kujitayarisha. Uliza kuhusu chaguo katika muji yako.

**2.** Sasa kwa kuwa unajua ginsi masomo inatumika kwa Finlande unavyofanya kazi, chora njia ile wewe ao mtoto yako ao jamaa anaweza kutumia. Zungumuza na umuulize mwalimu wako ikiwa una maulizo yoyote.




- Njia ya masomo ya ufundi kawaida ni haraka kuliko njia ya masomo ya juu, lakini kila moja ina faida yake. Zungumuza na shule yako, wafanya kazi wa ofisi ya kazi na utumishi ya kusimamisha jamii kuhusu chaguo zako.

# Majifunzo ya kujiingiza katika jamii kwa wahamiaji

Sasa kwa kuwa unajua ginsi masomo ya Finlande inatumika kwa ujumla, itakuwa namna gani wakati ile mhamiaji mtu mzima anapofika Finlande akiwa na ao bila masomo ya mbele kutoka inchi ingine? Utapata kujua hii, hata hivyo kabla ya kuanza kuna swali muhimu sana ile inahitaji kujibiwa.

**1.** Je, ungependa kufikia lengo gani linalohusiana na masomo ao kazi?

Sasa hebu tusome maandishi haya yafuatayo kwa pamoja.

Baada ya kufika inchini, wahamiaji wanaandikishwa katika mpango wa majifunzo ya kujiingiza katika jamii, ile inakuwa pamoja na masomo ya luga ya Kifinlande, masomo ya kijamii, hatua za maisha ya kila siku, maarifa ya kitamaduni, na vile vile ushauri wa kusoma na ushauri kwa masomo zaidi na kazi. Ao, mpango huo unaweka vipindi vya kujifunza katika nafasi ya kazi.

**2.** Unazani ni nini kinachohitajika ili kufikia lengo lako? Weka alama ya mviringo kwa mambo yale unafikili zinahitajika.

luga ya Kifinland | masomo ya kijamii | hatua ya maisha ya kila siku | kujua utamaduni | ushauri wa masomo zaidi na kazi | kujifunza | mpango wa kibinafsi wa masomo zaidi

**3.** Je, kuna kitu kingine unazani kinahitajika ili kufikia lengo lako?

# Masomo ya ufundi na majifunzo kwa watu wazima na majifunzo ya soko ya kazi kwa watu wazima

Kama tu ilivyo kwa wahamiaji vijana, wahamiaji watu wazima wanaweza pia kuomba masomo ya ufundi na majifunzo ili wapate kujua ufundi unayohitajika katika masoko ya wafanyakazi wa Finlande. Mwombaji anastahili kuomba kazi ikiwa ana cheti kutoka shule ya jumla ao cheti sawa cha masomo. Kiwango ya kutosha katika luga ya Kifinlande pia unahitajika. Kumbuka kufika na vyeti vyako kamili ya masomo ikiwa unavyo. Inafaa watu wakamilishe masomo ya ufundi inchini Finlande, kwa sababu inaimarisha bahati ya wahamiaji katika soko ya kazi.

Wahamiaji wasio na kazi, wale wamemaliza majifunzo ya kujiingiza katika jamii na kufikia kiwango cha luga ya Kifinlande kinachohitajika kwa masomo ya ufundi, wanastahili majifunzo ya soko ya kazi. Majifunzo ya soko ya kazi yanatazamia maisha ya kufanya kazi na yanaongeza masomo mbalimbali, na mara nyingi yanapeleka kustahili kamili ao kwa sehemu kwa ufundi

---

1. Je, ni masharti gani mawili yanayohitajika ili kuomba masomo ya ufundi inchini Finlande?

---

2. Kwa nini inapendezwa watu wakamilishe masomo ya ufundi?

---

3. Nani anastahili majifunzo ya soko ya kazi?

---

4. Je, majifunzo ya soko ya kazi mara mingi inapeleka nini?

---

5. Hapa chini unaweza kupata taratibu ya malengo. Chagua zile ambazo unapendelea na ukadirishe muda ile unafikili itachukua kuyafikia.

   **a.** Kujifunza Kifinlande | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

   **b.** Kujifunza Kiswidi | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

   **c.** Kujiandikisha katika mpango wa ufundi ya matayarisho | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

   **d.** Kujiandikisha katika programe ya masomo ya ufundi | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

   **e.** Kujiandikisha katika programe ya masomo ya kwanza | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

   **f.** Kujiandikisha katika programe ya masomo ya juu | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

   **g.** Kupata majifunzo yangu ya kwanza ya kujifunza | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

   **h.** Kupata kazi yangu ya kwanza | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

   **i.** Kuanzisha kampuni yangu mwenyewe | miezi(miezi)/mwaka(miaka) ______

# Kutambua masomo na diplome zilizokamilishwa inje ya nchi

Ikiwa una kiwango ya masomo kutoka inchi ingine, unaweza kuomba itambulike inchini Finlande. Unaweza kusoma kuhusu Shirika la Kitaifa la Masomo la Finlande, wapi unaomba masomo yako itambulike kwa oph.fi/english/services/recognition ao kwa kusoma alama ifuatayo ya QR.

**1.** Tayari wapi unapokuwa sasa, kuna jambo moja muhimu sana unalohitaji kukumbuka kuhusu kiwango ya masomo na vyeti. Hebu tulivumbue kwa kukamilisha aya ifuatayo na maneno yanayokosekana.

Ni muhimu ufike na nakala (copie) ______________ ao zilizohakikshwa za masomo ya msingi, ufundi ______________, programe za ______________ na ______________ ya kazi katika Finlande. Ni bora kufanya nakala hizi ______________ na kutafsiriwa katika ______________ tayari sasa.

ile ulizoea | masomo | kiwango ya masomo | halisi | Kizungu | kuhakikishwa

- Wahamiaji watu wazima wana majifunzo ya kujiingiza katika jamii na ushauri
  kwa masomo zaidi na kazi, na pia kujifunza.
- Masomo ya ufundi ili kuandisha kujua kwako kufikia sifa za soko ya kazi, pia inapatikana kwa wahamiaji watu wazima.
- Ikiwa una vyeti vyovyote, vitafsiri na kuja nazo kwa Finlande.

# Pahali pa kusoma vitabu na shuruli zaidi

Miji mingi inchini Finlande zina makubaliano ya jamii, yaliyo wazi kwa wenyeji wote. Unaweza kuomba vitabu ao k.m. usome gazeti tofauti katika luga tofauti bila malipo. Unaweza kutumia internet na usome pia kwa pahali pa kusoma vitabu. Lazima uombe kadi ya pahali pa kusoma vitabu ili uweze kuomba vitabu.


**1.** Hebu tujue ni wapi unaweza kupata pahali pa kusoma vitabu kwa Finlande. Enda kwa site ya hakemisto.kirjastot.fi ao utembelee site kwa kusoma alama ifuatayo ya QR.

**2.** Je, ni mambo gani unapenda? Je, unazani jambo ile unapenda inafanywa kwa Finlande? Ikiwa jambo unalopenda halipatikani inchini Finlande ao katika muji yako mpya, je, uko tayari kuanzisha kikundi wewe mwenyewe?

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________




Sasa kwa kuwa umekamilisha sehemu, hebu tufupishe kile ulichojifunza.



**Kazi ya kuongeza!**
Jaribu kujua ni wapi unaweza kufanya jambo lile unapenda kwa harrastushaku.fi ao kwa kusoma alama ya QR. Ikiwa unahitaji usaidizi kwa luga ya Kifinlande, omba usaidizi kutoka kwa mwalimu, mwenzako ao mshauri wako.

- Namna ya masomo inchini Finlande ni moja ya namna bora zaidi ulimwenguni. Weka lengo lako la kibinafsi na ujifunze vizuri ili uwe na mafanikio unayotaka katika maisha yako.

# Majibu

## Utumishi ya utunzaji ya watoto ya mchana na masomo ya mbele

**1.** Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| a. | b. | c. |
|---|---|---|
| mwaka moja | inategemea mapato ya familia | shuruli za ndani na inje |

## Shule ya jumla

**1.** Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| | | |
|---|---|---|
| a. | Uongo | Masomo ya msingi ni lazima kwa watoto wote wanaoishi inchini Finlande. |
| b. | Uongo | Masomo ya lazima ni kwa daraja za 1 hadi 6 na 7 hadi 9. |
| c. | Ukweli | Wazazi wana mapashwa ya kuhakikisha watoto wao wanahuzuria shule. |

**2.** Majibu yanaweza kupatikana kwenye ubao ifuatayo.

| a. | b. | c. | d. |
|---|---|---|---|
| w. | y. | x. | z. |

**3.** Majibu yanatofautishana, hata hivyo kumbuka kuwa kufundisha kwa Kifinlande inasaidia katika maendeleo ya kujua wa luga na inatayarisha wanafunzi vizuri zaidi kwa fasi zaidi za masomo.

**4.** Majibu yanatofautishana. Zungumuza mawazo ile na wakubwa wa shule. Kwa jumla, mafundisho ya kidini kwa Finlande yanalenga kufundisha kimakusudi kuhusu historia ya dini na desturi zake. Mafundisho ya tabia nzuri pia yanapatkana kwa ujumla.

**5.**

**a.** Wasichana na wanaume wanasoma pamoja Hii ni jambo nzuri kwa sababu mingi. Kwa jumla, hakuna kutenganisha kati ya jinsia katika jamii ya Finlande.

**b.** B. Wanafunzi wanatumia jina ya kwanza ya mwalimu inchini Finlande. Hii ni jambo nzuri kwa sababu inaondoa namna ya ukubwa, ile haionekane sana katika jamii ya Finlande kwa jumla. Kutumia jina ya kwanza ya mwalimu haimaanishi kuwa unamkosea heshima.

**c.** C. Kwa Finlande wanafunzi wanakula chakula cha mchana shuleni wakati wa mapumziko ya chakula cha mchana. Hii kawaida ni jambo nzuri kwa sababu mingi. Katika shule fulani, chakula inatolewa na uzuri wa chakula unafuatiliwa vizuri. Ikiwa una maulizo yoyote ya malisho, fahamisha uongozi.

**d.** D. Azabu kwa njia ya kimwili inakatazwa inchini Finlande. Hii ni vizuri kwa sababu hakuna mtu aliye na haki ya kumuazibu mtu mwingine kwa njia inayomutesa. Azabu inategemea hali na aina ya tabia mbaya.

**e.** E. Wazazi anafuatilia maendeleo ya kimasomo ya watoto yao inchini Finlande. Hatua hii ni nzuri kwa sababu inaruhusu wazazi kufahamu kuhusu masomo ya watoto wao na kuwasaidia.

**f** F. Wanafunzi hawasimami wakati mwalimu anapoingia. Hii ni nzuri kwa sababu inaondoa mafikili ya ukubwa. Unaweza kuwa mwenye heshima kwa mwalimu wako kwa kujifunza na kusaidia wakati wa masomo.

**g.** G. Wanafunzi hawavai nguo za shule inchini Finlande. Jambo hili ni nzuri kwa sababu kutokuwa na uwezo wa kununua nguo za shule haiwezi kuzuia uwezo wako wa kuenda kwa shule, na kwa sababu wanafunzi wako huru kuvaa ile wanataka ila tu inafaa kwa mazingira ya shule na hali ya hewa.

**h** H. Siku za kusoma katika shule ya jumla sio zaidi ya masaa sita kwa siku kwa ujumla. Jambo hili ni nzuri kwa sababu mingi, sawa wanafunzi kuwa na wakati wa shuruli zingine.

**i** I. Kuogelea kawaida ni sehemu ya programe inchini Finlande. Jambo hili ni nzuri kwani inasaidia mazoezi ya kimwili. Hatua za kuogelea ni muhimu inchini Finlande kwa sababu ya idadi ya maji kubwa na kukuwa na bahari. Ikiwa una wasiwasi chochote kuhusu hii, zungumuza na shule.

**6.**
**a.** A. Mara moja mjulishe mwalimu wako. Usiongoje ao kutumainia hali hii itakuwa bora.
**b.** A. Panga mkutano na fika kwa wakati.
**c.** C. Daima uliza ikiwa jambo sio wazi.
**d.** D. Mjulishe mwalimu wako mara moja.
**e.** E. Daima ni vizuri kukutana na watu wapya. Ikiwa una nia ya kula pamoja basi fanya hivyo, kataa ingine kwa hekima na kwa heshima.

**7.**
**a.** A. Panga mkutano na fika kwa wakati.
**b.** B. Usizuie mtoto wako kuhuzuria. Julisha usimamizi kuhusu wasiwasi yako.
**c.** F. Usiazibu mtoto wako. Zungumza na mtoto wako. Zungumuzia wasiwasi yako na mwalimu.
**d.** F. Usiazibu mtoto wako. Zungumza na mtoto wako. Zungumuzia wasiwasi yako na mwalimu.
**e.** E. Leta zawadi na umtie moyo mtoto wako.
**f** F. Usiazibu mtoto wako. Zungumza na mtoto wako. Zungumuzia wasiwasi yako na mwalimu.

## Shule ya sekondari ya juu

1. Shule ya sekondari ya juu ni kisha ya shule ya jumla.
2. Shule ya sekondari ya juu inachukia miaka 2 hadi 4.
3. Shule ya sekondari ya juu ni sharti kwa masomo ya masomo ya juu.

## Majifunzo ya ufundi

1. Kisha kumaliza masomo ya jumla, mtu anaweza kuchagua ao shule ya ufundi ao shule ya sekondari ya juu.
2. Masomo ya ufundi ni pamoja na vitendo sana. Wanafunzi wanafuata majifunzo mengi na masomo ya vitendo katika sehemu tofauti za kazi.
3. Ikiwa kijana mhamiaji anahitaji masomo zaidi ya luga ya Kifinlande ao Kiswidi o masomo mengine ya msingi, anaweza kufuata daraja la 10 katika masomo ya jumla ao mwaka moja katika majifunzo ya ufundi ya matayarisho.
4. Majibu yanaweza kupatikana kwekwa ubao ifuatayo.

| | a | b | c | d |
|---|---|---|---|---|
| Majifunzo ya ufundi kwa watu wa Finlande na wahamiaji | × | | × | |
| Majifunzo ya ufundi ya matayarisho kwa vijana wahamiaji | × | × | × | × |

5. Zote mbili; kisha ya masomo ya ufundi unaweza kuanza kufanya kazi mara moja ao pia kusoma zaidi.

## Masomo ya juu na vyuo vikuu

1. Majibu yanaweza kupatikana kwenye meza ifuatayo.

| a. | b. | c. |
|---|---|---|
| Uongo | Uongo | Ukweli |

2. Majibu yanatofautishana kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi.

## Majifunzo ya kujiingiza katika jamii kwa wahamiaji

1. Majibu yanatofautishana kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi.
2. Majibu yanatofautishana. Hata hivi, kumbuka kuwa juhudi nyingi zinahitajika na kujua luga ndio jambo muhimu katika kusoma na kufanya kazi inchini Finlande.
3. Majibu yanatofautishana kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi.

## Masomo ya ufundi na majifunzo kwa watu wazima na majifunzo ya soko ya kazi kwa watu wazima

1. Masharti ni kuwa na cheti kutoka shule ya jumla ao cheti hakika ya masomo, na pia kujua ya Kifinlande kadiri ya kutosha.
2. Ni vizuri watu wamalize majifunzo ya ufundi inchini Finlande kwa sababu inaimarisha bahati ya wahamiaji katika soko ya kazi.
3. Wahamiaji wasio na kazi, wale wamemaliza majifunzo ya kujiingiza katika jamii na wanajua Kifinlande vizuri wana haki kwa majifunzo ya soko ya kazi.
4. Majifunzo ya soko ya kazi mara mingi inapeleka kutambulika kamili ao kwa sehemu kwa kazi ufundi.
5. Majibu yanatofautishana kulingana na ile unapenda ya kibinafsi.

## Kutambua masomo na diplome zilizokamilishwa inje ya nchi

**1.** halali | masomo | diplome | ile ulijua | kuhakikisha | Kizungu

## Pahali pa kusoma vitabu na shuruli zaidi

1. Majibu yanatofautishana kulingana na eneo lako.
2. Majibu yanatofautishaana kulingana na ile unapenda ya kibinafsi na eneo lako. Unaombwa uanzishe kundi mpya ya kufanya jambo ile unapenda.
3. Majibu yanatofautishana.

# Kazi

**Kufanya kazi inchini Finlande**



Je, utafutaji kazi ni tofauti nchini Finlande? Je, aina ya kazi ni tofauti? Katika somo hili utajifunza kuwa kufanya kazi inchini Finlande nahitaji kujua luga ya wenyeji na juhudi za kibinafsi.

**Katika sehemu hii, utajifunza kuhusu:**

- Mpango wa kujiingiza katika jamii
- Majifunzo kwa wahamiaji
- Kutafuta kazi
- Ushuru
- Mapashwa na haki zako
- Utamaduni ya kazi


**Soma kuhusu sehemu hii katika mof.fi/sections/employment/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

**Pata sehemu hii mtandaoni katika mof.fi/exercises/employment/en ao usome alama wa QR ulio hapo chini**

# Mpango wa kujiingiza katika jamii na majifunzo kwa wahamiaji

Ni muhimu kufahamu kwamba luga katika mazingira ya kazi ya Finlande ni ya muhimu sana katika luga ya Kifinlande. Nafasi ya kazi api luga ya kazi ni Kizungu au luga ingine ya kigeni ni machache sana. Ili upate kazi inchini Finlande, lazima ujifunze luga hiyo. Ni ya faida kwako kuanza kujifunza luga tayari mbele ya kuhamia Finlande ili kuharakisha mwendo wa wako ya kujiingiza katika jamii.

1. Andika kazi zile ungependa kufanya na pia maelezo mafupi kuhusu kazi hizo kwa sehemu hizi.
2. Je, unahitaji kujua nini kwa kupata kazi hizi? Andika ile unataka kujua.



- Ili kupata kazi inchini Finlande unahitaji kujifunza luga, kujifunza mamboa mpya, na juhudi ya kibinafsi.

Ili upate kazi ile unataka, utakutana na changamoto mingi.
Ili kushinda changamoto hizi, unahitaji kujua na kuwa na maarifa kuhusu namna za kupata kazi kwa Finlande, katikati ya mengine.

**3.** Hapa chini unaweza kupata mifano ya masharti ya kimsingi ya kupata kazi inchini Finlande. Linganisha masharti haya na kujua ulioandika katika swali lililopita.

| **Masharti** | X |
|---|---|
| Kujua luga ya Kifinlande | |
| Vyeti rasmi vilivyohakikishwa | |
| CV inayokuwa na yale umejua na yale ulifanya na ombi ya kazi katika luga ya Kifinlande | |
| Masomo ya kufaa katika ile unataka kufanya ao kamili kwa kazi hiyo | |
| Ile umejua tayari kupitia kazi katika ile unataka kufanya ao kamili kwa kazi hiyo | |
| Uhusiano ya kijamii | |

**4.** Kwa maoni yako, ni rahisi kwa kiasi gani kupata kazi unayotaka? Je, unaweza kufikilia kuanza na kazi zingine zile zinakupa kujua mambo mapya na kujenga ufundi yako kutoka hapo?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Je, una maulizo zaidi kuhusu kazi zingine na masharti zake?
Jisikie huru kuuliza mwalimu wako.

!

- Kabla ya kupata kazi ile unataka, utahitaji kusoma vizuri na kufanya kazi nyingine nyingi. Mpango wa kujiingiza katika jamii itakusaidia.

Hebu tusome maandishi yafuatayo na tujibu maulizo mbalimbali. Toleo ndefu la maandishi haya pia linaweza kupatikana kwa ukurasa ya site ya somo, na kiungo cha ukurasa huu ya site kinaweza kupatikana kwa kurasa za kwanza ya ehemu; inakaa hivi mof.fi/sections/employment/en.

Unapozoea muji yako, ujiandikishe katika Ofisi ya Kazi na Maendeleo ya Uchumi (ofisi ya TE) katika eneo lako kama mwenye kutafuta kazi. Kama sehemu ya wakimbizi wanaohamia inchi ya tatu una haki ya mpango wa kujiingiza katika jamii kwa miaka mitatu ya kwanza ya kuishi inchini Finlande. Hii ni pamoja na masomo ya luga, kujifunza, majifunzo ya matayarisho ya maisha ya kazi, na majifunzo ya ufundi. Kwanza, kupima ha kwanza kitafanywa kulingana na historia ya masomo, ile umejua katika kazi, na hatua yako ya luga. Wahamiaji watu wazima kawaida wanaanza mpango yao ya kujiingiza katika jamii kwa kipindi cha majifunzo, ile ianhusu luga. Ikiwa kuna watoto wadogo nyumbani, mpango ya majifunzo ya kujiingiza katika jamii ile inaweza kubadilika itatolewa kwa mama.

**5.** Jina la Ofisi ya Kazi ni gani?

**6.** Jina ya mpango ile utashiriki kwa kujitayarisha ni gani? Taja hata sehemu mbili za mpango huu.

**7.** Je, utaulizwa nini wakati wa kutayarisha mpango?

**Kazi ya kuongeza!**
Hebu tutembelee site ya ofisi ya TE katika te-palvelut.fi ao kwa kusoma alama ifuatayo ya QR.

# Kutafuta kazi

Katika zoezi hili, utaunda CV. Hebu tuanze kwa kusoma maandishi.

---

Kutafuta kazi inchini Finlande inahitaji bidii ya kibinafsi na kuunda uhusiano ya kijamii, na wahamiaji wanasaidiwa katika hatua hii. Watu wa Filnlande na wahamiaji anaanza kazi zao kwa kufanya kazi zile zinasaidia kupata mapato wakati huo huo wakiunda uhusiano na kukamilisha kujua kwao. Mbel ya kukwenda kwa mahojiano yako ya kazi na kupata kazi yako ya kwanza, inawezekana kabisa utahitaji kutuma maombi ukitumia CV.

CV ina maelezo kuhusu masomo yako, historia yako ya kazi, na pia ile unajua. Ikiwa hauna historia ya kazi kamili, bado unaweza kuweka mambo yale unajua ya kazi isiyo kamili, kama vile ile unajua sawa kuchunga watoto ao kusimamia nyumba. Habari kukuhusu inapaswa kuwa katika Kifinlande. Katika maeneo mengine inchini Finlande, utahitaji kiandika katika Kiswidi. Unaweza kupata mifano mingi ya namna ya kuandika CV kwa Kifinlande kwa kutafuta "ansioluettelo" ao kwa Kiswidi kwa kutafuta "meritförteckning" kwa internet. Katika zoezi hili, mfano umetolewa kutoka kwa ansioluettelo.net ili uweze kuona ginsi CV rahisi inavyoonekana katika Kifinlande.

---

Ukurasa unaofuata una mfano wa CV. Hebu tuuangalie na tusome maulizo ili kuujaza.

**1.** Anza kuandika CV kwa kuandika maelezo ya kibinafsi. Hii ni pamoja na jina lako, tarehe ya kuzaliwa, adresse, na habari kuhusu namna gani kuzungumuza nawe.

**2.** Katika sehemu inayoitwa "työkokemus", andika historia yako ya kazi. Kwa mfano, mtu huyu alifanya kazi katika Nakkikioski Ry kati ya Februari 2002 na Juni 2007 kama mwenye kuuzisha, ao "myyjä" katika Kifinlande.

- Na wewe namna gani? Je, una ile unajua kutoka kwa kazi ya mbele?
- Andika tarehe, jina ya mwenye kazi, kile ulichokuwa unafanya huko, na ikiwezekana maelezo mafupi ya mapaswa yako. Jaribu kukumbuka chochote ile unajua kuhusu kazi hata kama inaonekana kama sio muhimu, kwa mfano majifunzo ya mwezi moja katika pahali pa kukata nywele, ao kufanya kazi kwa kutaka kwa miezi fulani kama mpishi pahali watu wanasaidiwa, ao kitu kingine chochote.
- Ikiwa hauna chochote ile umejua kutoka kwa kazi ya mbele, usiwe na wasiwasi. Bado kidogo utaweza kuongeza majifunzo na sehemu za kazi zile utapata katika pahali pako mpya ya kuishi.

**3.** Sehemu ya "koulutus" ni sehemu wapi unaandika historia yako ya masomo. Ulisomea nini? Ulisomea wapi? Andika majina ya shule ulizosomea pamoja na diplome ulizopata. Katika mfano wa CV, mtu huyu kati ya Agosti 2007 na Mei 2010 alihuzuria shule ya upili ya Mallila, yaani "Mallilan lukio" na kukamilisha kama mwenye alimaliza shule ya upili ao "ylioppilas".
Ikiwa hauna masomo yoyote kamili, unaweza kuacha sehemu hiyo ikiwa tupu kwa sasa.

**!**

- Wale wanachukua watu kwa kazi kwa Finlande watona kwa udamani ya maarifa yako katika kuandika na kuzungumuza Kifinlande.

**Etunimi Sukunimi**
Syntynyt 1.1.1900
Esimerkkitie 1
00000 KUNTA
Puh. 000 123 4567
etunimi.sukunimi@email.com

**ANSIOLUETTELO**

05.05.2015

---

**PROFIILI**

**TYÖKOKEMUS**

| | |
|---|---|
| 09/2014 - | **Yritys Oy**<br>Titteli / työtehtävä<br>Tarkempi kuvaus työtehtävistä. Voit myös kertoa saavutuksistasi tai työssä hankkimastasi erityisosaamisesta. |
| 02/2002 - 06/2007 | **Nakkikioski Ry**<br>Myyjä |

**KOULUTUS**

| | |
|---|---|
| 08/2010 - 05/2014 | **Oppilaitos**<br>Tutkinto |
| 08/2007 - 05/2010 | **Mallilan lukio**<br>Ylioppilas |

**KURSSIT**

Hygieniapassi, myönnetty 1.1.2008

**KIELITAITO**

| | |
|---|---|
| suomi | äidinkieli |
| englanti | erinomainen |
| ruotsi | perusteet |

**IT-TAIDOT**

| | |
|---|---|
| Microsoft Word | Hyvä |
| Microsoft Excel | Perusteet |
| AutoCAD | Erinomainen |

**HARRASTUKSET**

Kuntosali, lenkkeily

**SUOSITTELIJAT**

**Erkki Esimerkki, Esimies, Yritys Oy**
Erkki toimi esimiehenäni työskennellessäni Yritys Oy:ssä ohjelmistokehittäjänä.
Puh: 040 123 4567, sähköposti: erkki.esimerkki@yritysoy.fi

4. Kwa Finlande, “Hygieniapassi” ao Pasipoti ya Usafi, ile inaweza kusomwa katika sehemu ya "kurssit" ya CV kwa mfano ni lazima kwa mtu yeyote anayetaka kufanya kazi katika mikahawa (restora) na upishi, katikati ya sekta zingine.
   - Na wewe namna gani? Mbali na shule ulizofuata, je, ulifanya masomo ao majifunzo mengine yoyote? Uyaandike

5. Sehemu ya "kielitaito" ni ya luga. Je, unaweza kukisia ni luga gani?

| | |
|---|---|
| suomi | Kizungu |
| englanti | Kifini |
| ruotsi | Kiswidi |

   - Kwanza andika luga unazojua.
   - Kulia, unaona "äidinkieli", "erinomainen", na "perusteet”. Neno "äidinkieli" linamaanisha luga ya asili, na linaongeza "äidin" na "kieli". Unaweza pia kupata neno "kieli" kwa jina ya sehemu hii, "kielitaito", ile inamaanisha "kujua luga". Maneno "erinomainen" na "perusteet" yanamaanisha mtawaliwa "hatua" na "msingi".
   - Sasa andika kiwango cha ginsi unavyojua luga hizo.

6. Katika mfano unaweza kusoma "Microsoft Word" na "MicrosoftExcel". Hizi ni programe za kompiuta zinazotumiwa kuandika na kupanga vitu katika, katikati ya zingine. Kujua programe hizi ni kawaida sana inchini Finlande. Kwa upande mwingine, AutoCAD ni programe ya kufanya mambo mapya. Kulingana na maelezo haya unaweza kukisia IT-Taidot inamaanisha nini? Inahusu kujua unayohusiana na kompiuta. Kumbuka kuwa katika hali mingi kama sio zote, utalazimika kutuma CV kupitia barua pepe.
   - Sasa andika mambo yote yale unajua kuhsu kompyuta.

   Kwa kuume, unaona maneno yale yana udamani kwa kiwango cha kujua kwako. Mbali na maneno uliyoyasoma hapa mbele, neno "hyvä" linamaanisha vizuri.
   - Sasa andika kiwango cha hatua yako kwa kila jambo ile unajua.

7. Je, una jambo ile unapenda na shuruli unayofanya wakati una muda? Je, unapenda kusuka ao kucheza sataranji? Je, unapenda kuchezea mashine ao kusoma? Andika kwa "harrastukset".

8. Kwa mwisho, andika majina ya watu wale wanajua kazi yako ao watu wali ulifanya kazi nao mbele kwa sehemu ya "suosittelijat".

9. Hongera! Sasa una mfano wa CV ya msingi.

**Kazi ya kuongeza!**
Mbali na CV, barua ya kusukumwa kawaida inatumwa. Hebu tutembelee ansioluettelo.net tena na tutafute neno "työhakemus" ili tuone barua ya kusukumwa. Jaribu kutafuta katika internet ili kupata mifano mingine.

!

- Ili upate kazi unaweza kuhitaji kujifunza mambo mapya ao kuongeza kujua uliopata mbele ya kufika Finlande. Hii inaweza kuchukua muda, lakini kila juhudi itakusaidia kupiga hatua ya kupata kazi.

Mbali na kuwa na kujua ya kisasa, kuna mambo mengine yale yanakusaidia wakati unapotafuta kazi. Acha tupate maelezo zaidi kuhusu ginsi unaweza kuongeza ginsi unatafuta kazi

**10.** Je, ulitafuta kazi katika inchi zingine mbali na Finlande? Ulipata kazi? Ulipata kazi hiyo namna gani?

______________________________________________

______________________________________________

**11.** Kwa maoni yako, njia ya haraka zaidi ya kupata kazi ni gani?

- **a.** Ofisi ya kazi
- **b.** Marafiki
- **c.** Matangazo ya kazi
- **d.** Internet
- **e.** Mashirika ya kazi ya kibinafsi

**12.** Je, unaamini kuwa njia bora ya kupata kazi katika eneo lako la sasa na Finlande zinafanana?

______________________________________________

**13.** Je, unajua njia zingine za kupata kazi? Je, wewe ao mtu unayemjua ameanzisha biashara yake hapa mbele?

______________________________________________

**14.** Je, unaamini ni kazi ngapi zinachukua watu kupitia uhusiano ya jamii?

- **f.** 5%
- **g.** 25%
- **h.** 45%
- **i.** 65%
- **j.** 85%

**15.** Ingekuwa namna gani ungeambiwa kwamba asilimia hii ni 85%? Je, unazani hii ina maana gani kuhusu uhusiano ya jamii?

______________________________________________

______________________________________________

**16.** Je, unaundaje uhusiano wako katika inchi mpya wapi haujui luga yake vizuri? Zungumuza na wenzako.

______________________________________________

**!**

- Mtandao ni moja ya vitu muhimu zaidi wakati wa kutafuta kazi.
- Mtandao itasaidia wengine kujua uzuri ya kazi yako na kukusaidia ujifunze Kifilande.
- Watu wengi inchini Finlande wanachagua kujitumikia: Mtandao ni muhimu sana pia katika hali hii.

# Ushuru

Katika Finlande, kabla ya kuanza kazi yako, unahitaji kutoa Kadi ya Ushuru kwa mwenye anakupa kazi. Katika zoezi hili, unapata kujua zaidi kuhusu hili. Kwanza, hebu tuangalie mfano.

VERO SKATT
VEROHALLINTO

540A

MUUTOSVEROKORTTI 2013 1(2)
ÄNDRINGSSKATTEKORT 2013

Päiväys / Datum
06.11.2012

Verovelvollisen nimi
Den skattskyldiges namn

Henkilötunnus tai Y-tunnus
Personbeteckning eller FO-nummer

Kotikunta / Hemkommun 31.12.2012
475 MAALAHTI

Veronumero / Skattenummer

Tämä muutosverokortti korvaa 01.02.2013 voimaantulleen ja/tai aikaisemmin päivätyn verokortin
Det här ändringsskattekortet ersätter skattekortet som trädde i kraft 01.02.2013 och/eller tidigare

Ennakonpidätysprosentit voimassa 01.01.2013 - 31.12.2013
Förskottsinnehållningsprocent gäller 01.01.2013 - 31.12.2013

| | |
|---|---|
| Määräys koskee<br>Förordnandet gäller | palkkaa<br>lön |

| Perusprosentti<br>Grundprocent | Tuloraja<br>Inkomstgräns | Lisäprosentti<br>Tilläggsprocent |
|---|---|---|
| **12,5** | **9 800,00** | **26,5** |

Tulorajaan asti käytetään perusprosenttia. Ylimenevästä osasta ennakonpidätys toimitetaan lisäprosentin mukaan.
Grundprocenten används upp till inkomstgränsen. För den överskjutande delen verkställs förskottsinnehållningen enligt tilläggsprocenten.

Työnantajan merkinnät maksetuista suorituksista. Seuraavan työnantajan käytettävissä oleva tuloraja on verokorttiin merkitty tuloraja vähennettynä aikaisempien työnantajien maksamilla palkoilla.
Arbetsgivarens anteckningar om de betalda prestationerna. Inkomstgränsen som den följande arbetsgivaren kan använda är den på skattekortet antecknade inkomstgränsen minskad med lönerna som de tidigare arbetsgivarna utbetalat.

| Ajalta<br>För tiden | Työnantajan nimi<br>Arbetsgivarens namn | Bruttopalkat<br>Bruttolöner |
|---|---|---|

☐ Merkinnät ovat erillisellä liitteellä
Anteckningarna finns på en separat bilaga

Ohjeet kääntöpuolella
Anvisningar på baksidan

VEROH 0103a_T 11.2011

www.vero.fi
www.skatt.fi

Sasa tusome maandishi mafupi na tujibu maulizo.

Leo nilipokea simu wapi niliambiwa kwamba nimechaguliwa kwa kazi. Niliambiwa kwamba CV yangu ilikuwa nzuri, na mahojiano yangu ya kazi yalikwenda vizuri, na kwamba wale niliwataja walinishudia. Niliambiwa pia kwamba hatua inayofuata ni kupata kadi ya ushuru kutoka kwa ofisi ya ushuru ao kutoka kwa site ya ofisi ya ushuru vero.fi, na kuituma pamoja na namba yangu ya akaunti ya benki kwa mwenye alinipa kazi. Niliambiwa kwamba ikiwa sitatoa kadi ya ushuru, ofisi ya ushuru itapunguza mshahara yangu moja kwa moja kwa 60%. Nilichagua kupata kadi ya ushuru kupitia site kwa sababu inaokoa muda na pesa za usafiri. Kwenye site, niliweka kadiri ya mshahara na kisha nikachapisha kadi ya ushuru; haikuwa ngumu.

Nilikuwa na hamu, kwa hivyo nilipigia ofisi ya ushuru simu na kuwauliza ginsi wanavyohesabu kiwango cha ushuru. Walisema kuwa kiwango hicho ni kadiri na kwamba kinakatwa kutoka kwa mshahara yangu kiotomatiki, lakini kwamba baada ya mwisho wa mwaka nitaombwa kuangalia kiwango kamili cha pesa nilizopata na kujulisha ofisi ya ushuru, kisha watahesabu kiasi cha mwisho cha ushuru. Walisema kwamba ikiwa itatokea kwamba tayari nimelipa ushuru zaidi ya kiwango ambacho nilitakiwa kulipa, watanirudishia pesa, ama kwa njia ingine watanitumia facture kupitia barua, lakini kwa sababu tayari ninalipa kila mwezi kupitia punguzo la kiotomatiki, hata ikiwa kuna tofauti haifai kuwa kubwa; nilizani hili ni jambo nzuri. Hii ilionekana kuwa tofauti sana na inchi yangu, lakini napenda ginsi hatua hii imepangwa vizuri.

1. Kwa nini tunalipa ushuru?

2. Unapata Kadi ya Ushuru wapi?

3. Katika mfano wa Kadi ya Ushuru, ni asilimia ngapi ya ushuru ambayo ingelipwa kwa mwanzo ikiwa mapato ni chini ya yuro 9800?

4. Kwa mfano, ni asilimia ngapi ya kiwango ya ushuru ile ingelipwa kwa mwanzo ikiwa mapato ni zaidi ya yuro 9800?

5. Je, asilimia ya mwanzo ya ushuru uliokatwa ingekuwa ngapi ikiwa mfanya kazi hatatoa kadi ya ushuru?

6. Je, kiwango cha mwisho cha ushuru kinahesabiwa namna gani?

!

- Ushuru ni sehemu muhimu ya namna ya kusimamisha kijamii ya Finlande.
- Wakaaji wote wa Finlande wanalipa ushuru. Ushuru inawezesha usaidizi katika kujiingiza kwako katika jamii kama mkimbizi.
- Kulipa kodi yako ndio njia yako ya kuhakikisha mchango yako mzuri kwa jamii

# Mapashwa na haki zako

Wakati wa kuanza kazi yako mpya, ni muhimu kujua haki zako na kile ambacho wenye wamekupa kazi wanatarajia ufanye. Tembelea ukurasa wa somo ili usome maelezo marefu kuhusu haki na mapashwa zako. Maandishi hapa chini ni sehemu kutoka kwa ukurasa wa somo.

---

Wakati wa kuanza kazi mpya, makubaliano ulioandikwa inawekwa sahihi kati ya mwenye kuleta kazi na mufanya kaziwapi, wapi wanakubaliana kuhusu madaraka ya kazi, masharti, na malipo. Aina ya makubaliano inaweza kuwa ya kudumu ao kwa muda uliowekwa. Makubaliano inapaswa kuwa na mshahara, saa za kazi, kipindi cha kazi, na maelezo kuhusu madaraka kazini.

Ni muhimu pia kufuata ratiba inchini Finlande. Kwa jumla, wakati wote mtu anakuja kufanya kazi kwa wakati uliowekwa. 8:00 inamaanisha 8:00 kamili na sio 8:10. Kuchelewa inachukuliwa kuwa kukosa kujiheshimu, kwani watu wengine wanapaswa kusubiri mtu aliyechelewa.

